Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Udhuu Kwa Mtazamo Wa Qurani Na Sunna

### Author(s):

Sheikh Jafar Subhani [3]

### Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: kilichoandikwa na Sheikh Ja'far al-Subhani. Sisi tumekiita: "Udhuu kwa mtazamo wa Qur'ani na Sunnah" Kitabu hiki kinahusu Udhuu. Udhuu ni tendo la kunawa (kutawadha) kisheria kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Swala.

### Translator(s):

Sheikh Harun Pingili [5]

### Category:

General [6]

### Topic Tags:

Qur'an [7]
Swala [8]
Dini [9]
Sheria [10]

**Person Tags:**

Mtume Muhammad (s.a.w) [11]

# Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: kilichoandikwa na Sheikh Ja'far al-Subhani. Sisi tumekiita: "Udhuu kwa mtazamo wa Qur'ani na Sunnah"

Kitabu hiki kinahusu Udhuu. Udhuu ni tendo la kunawa (kutawadha) kisheria kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Swala. Swala ni nguzo kubwa ya dini haikamiliki mpaka mtu awe na Udhuu: "Enyi! ambao mmeamini mnapokusudia kuswali osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye viwiko, na pakeni sehemu za vichwa vyenu na miguu yenu mpaka kwenye nguyu mbili..."(al-Maidah; 5: 6).

Aya hii ni mojawapo ya Aya za hukumu ambazo humo huchukuliwa hukumu za kisharia kiutekelezaji inayorejea kwenye kunadhimu matendo ya wanaopasa kutenda katika ambayo yanaambatana na shughuli za maisha yao ya kidini na ya kidunia.

Bahati mbaya kuna tofauti ya jinsi ya kutawadha kati ya Shi'a na Sunni kiasi kwamba kila mmoja anamshangaa mwenzake, hususani mwiongoni mwa wafuasi. Wengi wa wanachoni wa Kisunni wamejuzisha kukosha miguu, ambapo wanachuoni wa Kishi'a wamejuzisha kupaka miguu.

Imekuwa in kawaida ya watu kukubali kila jambo linalofanywa na watu katika jamii wanayo ishi bila ya kuhoji ubaya au uzuri wa jambo hilo. laki- ni hii yote ni kwa sababu ya kutojuana na kutotaka kujuana.

Mwandishi wa kitabu hiki ameshughulikia suala hili kwa kutumia Qur'ani na Sunnah, vyanzo viwili ambavyo ndio chimbuko la sheria na hukumu zote za dini kwa madhehebu zote za Kiislamu, na akahitimisha kwa mujibu wa vyanzo hivyo viwili.

Kwa ajili hii tumeona tukitoe kwa lugha ya Kiswahili kwa wasomaji wetu wa Kiswahili ili wapate kunufaika na maudhui hii. Tunataraji kwamba wote watanufaika na somo hili na kutekeleza ibada zao kwa mujibu wa sheria.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Harun Pingili kwa kubali jukumu hili la kutarjum kitabu hiki. Halikadhalika tunawashukuru wale wote walioshiri- ki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701

Dar-es-Salaam, Tanzania.

# Udhuu Kwa Mtazamo Wa Qur'ani Na Sunna

Sifa njema ni za Allah (s.w.t.) Bw. Mlezi wa ulimwengu wote. Swala na salamu zimfikie mbora wa viumbe wake na hitimisho la mitume wake, Muhammad (s.a.w.w.) na ziwafikiye Aali zake wazuri wasafi ambao ni bweta la elimu yake na ni wahifadhi wa Sunna zake.

Kwa kweli Uislamu ni:

**a. Itikadi**
**b. Sheria**

Itikadi: Ni imani kumuamini Mungu, siku ya mwisho, na Mitume yake.

Sheria: Ni hukumu za kiungu ambazo zinachukua dhamana ya maisha yaliyo bora kwa ajili ya binadamu, na kumhakikishia furaha ya dunia na ya Akhera.

Na sheria ya kiislamu imemaizika kwa uenezi, na kuweka kwake imeju- likana wa matatizo yote yampatayo mwanadamu katika pande zote za maisha.

**Amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):**

الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ ۚ الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا ۚ {3}

***"Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimekutimizieni neema zangu na nimekuridhieni Uislamu kuwa dini yenu."* (*Al-Maidah :3:10 3*).**

Ila tu kuna masuala mbalimbali wanavyuoni wametofautiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu yaliyotoka kwa mfikishaji risala Mtume Mtukufu (s.a.w.w.).

Ni jambo ambalo limesababisha kutofautiana neno lao humo (katika masuala), na kwa ukweli tumejaribu katika masomo haya yaliyo katika mlolongo tuyawasilishe juu ya meza ya utafiti, huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha neno hili na kusogeza karibu hatua katika konde hili; hivyo basi tofauti iliyopo si katika kiini cha dini na misingi yake hata kusababishe uadui na chuki; bali ni tofauti kuhusiana na yaliyoelezwa kutokana na yeye (s.a.w.w.), na hilo ni jambo dogo kwa kulinganisha na masuala mengi yaliyo katika

muafaka kati ya madhehebu za kiislamu.

**Mfumbuzi wetu katika njia hii ni kauli yake (s.w.t):**

الْيَوْمَ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ ۚ الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا ۚ {3}

***"Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimekutimizieni neema zangu na nimekuridhieni Uislamu kuwa dini yenu."* (*Al-Maidah: 3:103*).**

**Sheikh Jafar Sub'haaniy**
**Taasisi ya Imam Sadiq,**
**Qum.**

## Aya Ya Udhu Ni Aya Muhkamah

Waislamu wameafikiana kwa mujibu wa na Kitabu kitukufu kuwa Swala haiwi sahihi isipokuwa kwa tohara, nayo ni: Wudhu, Josho, na Tayammum, na Allah (s.w.t.) amebainisha siri ya taklifu ni kwakuipata tohara kabla ya Swala kwa kauli yake:

(Mwenyezi Mungu hataki kuwafanyiyeni ugumu, lakini anataka kuwatoharisheni).
Udhu katika sheria ya kiislamu umepata umuhimu mkubwa kama ambavyo Qur'an na Sunna vimetamka. Amesema Mtume (s.a.w.w.): (Hapana Swala ila kwa tohara), na katika maneno yake mengine: (Wudhu ni sehemu ya imani) (*Al'wasaailu*, Juz.1, mlango wa kwanza miongoni mwa milango ya Wudhu).

Ikiwa hii ndio nafasi ya Wudhu basi ni wajibu kwa Muislamu kuzitambua sehemu zake, na sharti zake, na vitanguzi vyake na vibatilisho vyake. Vitabu vya *Fiq'h* vimebainisha umuhimu huu. Ambalo twalitilia mkazo hapa ni kubainisha lile ambalo neno la wanavyuoni limehitilafiana kwalo. Naikusudia hukumu ya miguu upande wa kuosha au kupaka, hivi basi twasema:

Mungu Mtukufu amesema ndani ya Kitabu chake kitukufu akibainisha wajibu wa wudhu na jinsi yake kwa kauli yake:

الْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبَاتُ ۚ وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حِلٌّ لَكُمْ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَهُمْ ۚ وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ ۚ وَمَنْ

يَكْفُرْ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ {5}

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ ۚ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ۚ وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ حَرَجٍ وَلَٰكِنْ يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ {6}

***“Enyi! ambao mmeamini mnapokusudia kusali osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye viwiko, na pakeni sehemu za vichwa vyenu na miguu yenu mpaka kwenye nguyu mbili, na endapo mkiwa na janaba jitoharisheni na muwapo wagonjwa au safarini au yeyote kati yenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake na hamkupata maji, hivyo fanyeni Tayamamu kwa mchanga safi. Pakeni sehemu za nyuso zenu na mikono yenu kwa huo* (*mchanga*)*. Mungu hataki kukutieni shida, lakini tu yuataka kukutoharisheni na kukutimizieni neema yake kwenu ili mpate kushukuru.* (*Al-Maidah; 5: 6*)*.***

Aya hii ni mojawapo ya Aya za hukumu ambazo humo huchukuliwa hukumu za kisharia kiutekelezaji inayorejea kwenye kunadhimu matendo ya wanaopasa kutenda katika ambayo yanaambatana na shughuli za maisha yao ya kidini na ya kidunia.

Na kipande hiki cha Aya kina ufafanuzi ulio wazi, na dalili iliyo safi, kwa kuwa anayeambiwa hapa ni umma wa waumini ambao wapenda kutekeleza kama ilivyo mwenendo wake wa kimatendo kulingana nazo (Aya). Kwa ajili hiyo zinatofautiana na Aya zinazoambatana na *tawhid* ya kina na maarifa ya kiakili, ambayo hufungiwa humo maoni ya wanafikra waliobobea, khususan katika ambayo yanaambatana na masuala ya chanzo na ufufuo.

Na mtu endapo atazizingatia Aya hizi na zilizo mfano wake, miongoni mwa Aya ambazo zinachukuwa dhamana ya kubainisha wadhifa wa muislamu, mfano wa kutekeleza Swala katika nyakati tano, atakuta maelezo yake ni thabiti, ubainifu wake uko safi, dalili yake ni ya wazi inayowasemesha waumini wote ili kuwachorea majukumu yao wakusudiapo kusali.

Na kauli ya tamko – kama ulivyokwishajua – kuwa yabidi liwe mbali na utata na ugumu, mbali na kutanguliza (neno au kucheleweshe, mbali na kukadiria jumla moja au neno, ili madhumuni yake wayaelewe Waislamu wote hali wakiwa wanatofautiana viwango vyao bila tofauti kati ya mjuzi wa kanuni za Lugha ya kiarabu na asiye mjuzi.

Hivyo basi mwenye kujaribu kuitafsiri Aya hii kwa utaratibu usiokuwa huu atakuwa ameghafilika mahali pa Aya na nafasi yake, kama ambavyo mwenye kujaribu kuitafsiri kupitia mwanga wa *fatwa* za kifiq'hi za maimamu wa *fiq'hi* atakuwa ameingia mlango usio wake.

*Ruhul'amiinu* Jibril aliiteremsha Aya hii kwenye moyo wa Bwana wa mitume, naye aliwasomea Waislamu na waliufahamu wajibu wao kuielekea Aya kwa uwazi kabisa, bila ya kutaradadi, bila ya kuingiwa na hali isiyoeleweka wala ugumu katika hiyo Aya. Isipokuwa utata ulijipenyeza kwenye Aya zama za mgongano wa rai na kujitokeza kwa ijtihadi (nyingi).
Hivyo mwenye kuisoma Aya hii iliyobarikiwa kwa mazingatio atasema moyoni mwake na ulimini mwake: *Sub'haanaka* maneno yako yana balagha ilioje na ubainifu wako una fasaha ilioje, umeweka wazi faradhi na kuubainisha jukumu la yale yaliyo wajibu kwa Muislamu kuyatenda kabla ya Swala, uliposema: (*Yaa ayyuha lladhiyna Aamanuu idhaa qumtum ila swalaati*). Kisha ukasema ukibainisha jinsi ya wadhifa ulivyo, kuwa ni mambo mawili:

( ***fagh'siluu wujuhakum wa aydiyakum ilal'marafiqi***)
(***wa msahu biruusikum wa arjulakum ilal'ka'abayni***)

Umetakasika haukubakisha maelezo ya jumla jumla ndani ya maneno yako, wala utata katika kubainisha kwako, kwa hiyo umeufunga mlango wa tofauti na umeziba mlango wa kutojali kwa kufafanua faradhi na kuibainisha.

Umetakasika Ewe Allah ikiwa Kitabu chako kitukufu ndio msimamizi wa vitabu vya mbinguni kama ulivyosema:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ ۚ {48}

***Na tumekuteremisha Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu na kuyalinda.*** (***Al-Maidah:48***)***.***

Hivyo basi Kitabu hiki ni msimamizi – kwa ithibati na yakini – wa riwaya zilizokuja katika athari kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) nazo ziko kati ya zinazoamrisha kuosha miguu na zinazoamrisha kuipaka.

Tufanye nini sasa na hizi riwaya zilizokuja katika athari zinazopingana zilizoelezwa kutoka kwa ambaye *la yantwiqu ila anil'wahyi*, hatamki ila kutokana na *wah'yi* wala hajipingi binafsi katika usemi wake? umetakasika hatuna upenyo isipokuwa kuyachukua yaliyonadiwa na Kitabu chako kitukufu na Qur'an Yako yenye enzi, na kwa hakika umebainisha katika jumla mbili zinazoweka wazi ukweli wa wajibu kuwa yafanyika kwa (viungo) viwili vya kuosha (*Fagh'siluu wujuhakum wa aydiyakum ilal'marafiqi*). (na osheni nyuso zenu na dhiraa zenu mpaka kwenye viwikozviwili). Kama unavyofanyika kwa (viungo) viwili vya

kupaka:

وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ ﴿6﴾

***Na pakeni sehemu za vichwa vyenu na miguu yenu mpaka kwenye nguyu* (*kiungo cha mguu na kanyagio*) *mbili.* (*Al-Maidah: 5: 6*)**

أَفَغَيْرَ اللَّهِ أَبْتَغِي حَكَمًا وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا ﴿114﴾

***"Je nimtake hakimu ambaye sio Mungu hali yeye ndiye ambaye amekuteremshieni kitabu – kifafanuzi."* (*Al'An'aam:114*)**

Umetakasika Mola wangu hujabakisha fumbo katika maneno yako wala utata katika kubainisha kwako, kwa hiyo umeufunga mlango wa mfarakano, na kuufunga mlango wa ujahili kwa kuuweka wajibu wazi na kuubainisha.

Umetakasika ewe Mola wangu, ikiwa Kitabu Chako kitukufu ndio kinachosimamia vitabu vya mbinguni kama ulivyosema:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ ﴿48﴾

***"Na tumekuteremshia kitabu kwa ukweli chenye kusadikisha yaliyokuwa kabla yake katika kitabu, na mchunga wa hivyo vitabu."* (*Al-Maidah; 5: 48*)**

Kwa hiyo ( hiki kitabu) ni mchunga – kwa (dalili) ya mkato na yakini – wa yaliyopatikana kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) nayo yapo kati ya yaamrishayo kuosha miguu na yaamrishayo kuipaka.

Sasa tutafanyaje na hizi habari zinazopingana zilizoelezwa kutoka kwa asiyetamka isipokuwa ni *wahyi* na wala hajitangui mwenyewe maneno yake?

Umetakasika hatuna kimbilio ila kuchukua ambalo Kitabu Chako kitukufu kimelinadi na kimebainisha katika jumla mbili zinazoweka wazi ukweli wa wajibu, kuwa unatimia kwa sehemu mbili za kuosha

(***fagh'siluu wujuhakum, wa aydiyakum ilal'marafiqi***)

Kama unavyotimia kwa sehemu mbili za kupaka:

(***famsahu biru'usikum wa arjulakum ilal'ka'abayni***)

أَفَغَيْرَ اللَّهِ أَبْتَغِي حَكَمًا وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا ۚ {6}

(***afaghayra'llahi abtaghi hakaman wahuwa lladhiy anzala ilaykumul'kitaba mufaswalan***) (***Al'an am: 6***)

## Mwanzo Wa Tofauti

Waislamu walikuwa wanaafikiana katika suala la Wudhu kabla ya enzi ya Khalifa wa tatu, wakati huo hapakuwa na tofauti yoyote iliyojitokeza kuhusu kupaka miguu miwili au kuiosha; bali tofauti ilianza wakati wa enzi ya khalifa wa tatu, kama inavyoonyesha katika riwaya nyingi za ubainifu zilizoelezwa na Seyydna Uthman. Na Muslim ametaja kundi miongoni mwazo ndani ya *Sahihi* yake.

1. Muslim ameitoa (kuieleza) kutoka kwa Humran, huria wa Uthmani amesema: "Nilimletea Uthman bin Affani maji, alitawadha, hati maye akasema:

"Kwa kweli watu wanaongea kuhusu Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) Hadith sijui ni zipi hizo? Tambua! Kwa hakika mimi nimemuona Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) akitawadha mfano wa wudhu wangu huu; kisha akasema: Mwenye kutawadha kama hivi, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia, na itakuwa Swala yake na kwenda kwake msikitini ni naafilah – Sunna."1

2. Ametoa Muslim kwa Abiy Anasi kuwa Uthman alitawadha kwa mgao na akasema: "Je nisiwaonyesheni wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)." Hatimaye alitawadha mara tatu tatu. Na Bw. Qutaybah amezidisha katika riwaya yake. Amesema Sufyani: Abu Nadhri amesema kutoka kwa Abiy Anasi amesema: Akiwa na watu miongoni mwa swahaba wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.).2

Na kuna Riwaya nyingine za kubainisha kwa ulimi wa Uthmani. Muslim hakuzieleza, lakini zimetajwa na wengine, zote zinaonyesha kujitokeza kwa tofauti kuhusu jinsi ya wudhu wa Mtume, kwamba kulikuwa katika zama zake (Othman), ***ama kuhusu nini sababu ya tofauti, ubainifu wake unakujia.***

## Qur'an Tukufu Ndio Msimamizi Na Rejea Pekee, Pindi Athari Zikitofautiana.

Qur'an tukufu ni msimamizi wa vitabu vya mbinguni. Nayo ni mizani ya (kuutambua ) ukweli na batili. Hivyo basi habari zitakazokuja humo (kati– ka vitabu vya mbinguni) huchukuliwa endapo hazitokhalifu Kitabu kituku– fu, vinginevyo zitapigwa ukutani.

Ikiwa huu ndio msimamo wa Qur'an Tukufu kuvihusu vitabu vya mbin- guni, ni bora zaidi iwe hivyo kuzihusu Sunna zilizotokana na Mtume (s.a.w.w.). Qur'an ni msimamizi wake, kwa hiyo Sunna hufanyiwa kazi - endapo sanadi itakuwa sahihi - ilimradi tu haipingani na Kitabu - Qur'an.

Wala hilo halimaanishi kutosheka na Qur'an na kuifutilia mbali Sunna kwa kuiweka kando na sharia, hiyo ni itikadi ya wazandiki. Sunna ni hoja ya Waislamu, ya pili-baada ya Kitabu kitukufu - kwa sharti Sunna ielezayo isipingane na sanadi ya uhakika kwa Waislamu.

Ikiwa Qur'an Tukufu imesema chochote kuhusu kupaka au kuosha, Sunna au habari inayoamrisha kinyume chake ina thamani gani! Na'am; Endapo yawezekana (Aljam'u) kuziowanisha kati ya Qur'an Tukufu na zile habari kwa kuichukua ya pili kuwa ilikuwa kwa muda tu wa wakati, kisha Qur'an ilifutilia mbali hivyo itakuwa ndivyo, kama sivyo naipigwe ukutani.

Bw. Ar-Raziy amesema: "Mtume (s.a.w.w.) amesema:

Endapo mmeelezwa Hadith basi ipimeni na Kitabu cha Mungu, ikiafikiana nacho ikubalini, ama si hivyo ikataeni.3

## Al-Maidah Ni Sura Iliyoshuka Mwisho

Kwa hakika Sura ya Al-Maidah ni Sura iliyoshuka mwisho kwa Mtume (s.a.w.w.), ndani yake hakuna Aya ambayo (imeondolewa hukumu yake). Ametoa (habari) Ahmadi, na Abu Ubaydi ndani ya kitabu chake:

*Al-fad- hwailu* na *an-Nuhasu* na ndani ya kitabu chake: *An-Naasikhu*, na *an-Nasaaiy* na Ibnul'Mundhir, na Al-Haakimu na Ibnu Mardawayhi, na al'Bayhaqiy ndani ya *SunNanu* yake kutoka kwa Jubayru ibni Nafiiru. Amesema: "Nilihiji nikaingia kwa (mama) Aisha akaniambia: Ewe Jubayru wasoma (sura ya) Al-Maaidah, nikasema: Naam, Akasema: Kwa hakika hiyo ni Sura iliyo shuka mwisho, hivyo basi mukutacho humo miongoni mwa halali kihesabuni kuwa ni halali, na mukikutacho humo miongoni mwa haramu basi kihesabuni kuwa ni haramu."

Na ametoa (habari) Abu Ubaydi, kutoka kwa Dhwamra bin Habiibu, na Aatiyatu bin Qaysi, wawili hao wamesema: "Amesema Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) kuwa: "Al-Maaidah ni ya mwisho kuteremka katika Qur'an, hivyo basi halal- isheni halali yake na haramisheni haramu yake."

Na ametoa (habari) Al-Fariabiy na Abu Ubaydi, na Abdu bin Hamiidi, na Ibin Al Mundhiri, na Abu Sheikh kutoka kwa Abu Maysarah, Amesema:

(***fil maidati thamaniy ashrata fariidhwata laysa fii Suratin minal'Qur'an ghairaha walaysa fiiha mansukhu, wa adda minha*** (***wa idha qum tum ilaswalati fagh'siluu***)

"Ndani ya Suratul-Maaidatu kuna faradhi kumi na nane hazipo katika Sura nyingine yeyote katika Sura

za Qur'an isio hii, wala katika hizo hakuna mansukhu (iliyoondolewa) na alizihesabu miongoni mwazo,

(***wa idha qumtum ila swalati fagh'siluu***).

Na Abu Daudi na An-Nuhaasi wametoa (habari) hao wote wawili katika An-Nasikhu kutoka kwa Abiy Mysarah Amru bin Sharhiil alisema: "Ndani ya Surati Al-Maidah hapajanasikhiwa (kuondolewa) kitu."

Na ametoa (habari) Abdu bin Hamidu alisema: "Nilimuuliza Hasan, Je katika Sura ya Al-Maaidah kuna kilichofutwa? Akasema: La, hapana."4

Hayo yote yanajulisha kuwa Surati Al-Maidah ni Sura iliyoteremka kwa Mtume mwisho, hivyo basi hakuna upenyo wa kuacha kutenda kwa mujibu wake wala haina naskhi – kilichoondolewa.

Riwaya kutoka kwa maimamu wa Ahlul-Bayt zimesaidiana (kuthibitisha) kuwa Sura ya Al-Maidah ni Sura iliyoteremka mwisho wala ndani yake hakuna Aya mansukhah – iliyoondolewa hukumu yake.

Muhammad bin Mas'udi Al'Ayaashiy As-Samarqandiy ametoa (habari kutoka kwa Ali (a.s.): "Qur'an ilikuwa baadhi yake inafuta baadhi nyingine. Huchukuliwa kutoka amri za Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) ile ya mwisho wake tu. Na ya mwisho iliyoteremka kwake ni Suratu Al-Maidah ilifuta zilizoshuka kabla yake wala yenyewe haikutenguliwa na kitu."5

Ametoa Shaikh Tusiy sanadi yake kwa Aswadiqu na Al-Baaqiru (a.s.), kutoka kwa Amirul-Muuminin Ali (a.s.) aliposema katika hadith ndefu:

Kwa mwanga huo lau kitabu kingejulisha chochote kuhusu kupaka na kuosha, fathari zinazotofautiana nacho, aidha zingefanyiwa ta'awili kuwa zimefutwa na Qur'an au hutupiliwa mbali.

## Chimbuko La Tofauti

Ikiwa mwanzo wa tofauti ni wakati wa enzi ya khalifa wa tatu, kuna swali lajitokeza lenyewe: Nini sababu ya tofauti katika suala la Wudhu, baada ya kupita taqriban miaka 20 toka kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi twasema: Kuna sababu na uwezekano kadhaa:

### 1. Tofauti Za Qira'ah

Huenda ikafanywa taswira kuwa chimbuko la tofauti katika zama zile ni tofauti ya usomaji kwa kuwa wasomaji wametofautiana katika irabu ya katika kauli yake (s.w.t.): Kuna ambao wameisoma kwa *jarri* wakiizingatia kuwa ni "Miguu imeunganishwa na kichwa katika hukumu ya kupaka kwa mujibu wa kiunganishi."

Na miongoni mwao kuna ambao wameisoma kwa *fat'ha* wakiizingatia katika kauli yake (s.w.t.) ambayo yalazimu ioshwe.

Kwa kweli mtizamo huu ni batili kabisa, kwa kuwa Mwarabu halisi aisomapo Aya akiwa mbali na rai nyingine yeyote hatoridhika (aisome Aya) bila ya kuiunganisha miguu na kichwa, sawa aisome kwa *nasbi* yaani *fat'ha* au *jarri* yaani *kisra*. Ama kuiunga na neno: *wujuuhakum* hilo halimjii mawazoni mwake hata iwe ndio chimbuko la tofauti.

Kwa hiyo mwenye kuitaka tafsiri ya Aya na kufahamu yajulishwayo na Aya hii ajifanye yeye mwenyewe kana kwamba yu katika zama zile za kushuka Aya na yuasikiliza maneno ya Mwenyezi Mungu kutoka kinywa cha Mtume Mtukufu (s.a.w.w.) au swahaba wake, kwa vile atakalolifa- hamu hapo ni hoja kati yake na Mola wake, hapo hatokuwa na haja ya kutegemea yawezekana hivi au vile! Na mitazamo tofauti ambayo haikuwa wakati ule na ilijitokeza baada ya wakati ule.

Lau tuilete Aya mbele ya Mwarabu aliye mbali na mazingira ya kifiq'hi na tofauti za Waislamu katika jinsi ya kuchukua wudhu, na tumuombe abain- ishe alilofahamu, angesema kwa wazi kabisa: Kwa kweli wudhu ni sehemu mbili za kuosha na mbili za kupaka bila ya kufikiria kuwa je miguu inaungwa na hukumu ya kichwa au inaungwa na hukumu ya nyuso?
Kwani yeye anadiriki kuwa hii (jumla) ndani yake mna jumla mbili zilizoeleza wazi hukumu mbili:

Kuanza na jumla ya kwanza:

(Osheni nyuso zenu na mikono yenu pamoja na *maraafiqi* (viwiko) ( *mir- faq* ni: kiwiko cha mkono, wingi wake ni *maraafiq*) kwa kuosha nyuso kisha imeunganishwa mikono hukumu moja na nyuso, hivyo, mikono ikawajibika kuwa na hukumu ile ya nyuso kwa sababu ya *at'fu* (kiungo) cha herufi *wau* ? .

Hatimaye ilianza jumla ya pili:

(Na pakeni baadhi ya vichwa vyenu na baadhi ya miguu yenu mpaka kwenye *ka'ab* mbili) kwa amri ya kupaka vichwa kisha akaiunga pamoja miguu (kwa amri hiyo hiyo hivyo basi ikawajibika kuwa na hukumu ile ya vichwa, kwa sababu ya *at'fu* yaani kiungo *wau*?, na *wau* yajulisha ushirikiano wa kile kinachokuja baada yake na kile cha kabla yake katika hukumu. Na kufarikisha kati ya hukumu ya vichwa na hukumu ya miguu hakutumainii Mwarabu halisi bali yuaona ni kinyume na dhahiri ya Aya.

## 2. Kushikilia Riwaya Ya Kuosha Iliyonasikhiwa

Yaonyesha kutokana na si moja miongoni mwa riwaya kuwa kuosha miguu miwili ilikuwa ni sunna, Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha muda fulani katika umri wake, na ilipoteremka Suratul'Maaidah ndanimwe mukiwa na Aya ya wudhu na amri ya kuipaka miguu miwili mahali pa kuiosha, kwa muda fulani - asiyejuwa *naasikhu* na *mansuukhu* aliichukuwa Sunna iliyonasikhiwa na kutimua (vumbi la) mfarakano akiwa ameghafilika kuwa wajibu wake ni kuifuata Qur'an iliyonasikhi Sunna. Ndani ya hiyo (Qur'an) kuna Suratul'Maaidah ambayo ni Sura ya mwisho iliyoteremka kwa Mtume (s.a.w.w.).

Ibn Jariri ametoa kutoka kwa Anasi amesema: "Qur'an ilishuka na *mas'hu* (kupaka), na Sunna ilileta *ghuslu* (kuosha)."6

Kwa Sunna, anakusudia tendo la Nabii (s.a.w.w.) kabla ya kushuka Qur'an. Na yajulikana kuwa Qur'an ni hakiimu na nasikhu. Na Ibin Abbas amesema: "Watu hawataki ila kuosha, na wala sikuti ndani ya Kitabu cha Mungu ila kupaka."7

Kwa mujibu huu yawezekana kuoanisha kati ya yaliyosemwa kutokana na tendo la Nabii (s.a.w.w.) la kuosha na kudhihiri kwa Aya katika kupaka, na kuwa kuosha kulikuwa kabla ya kuteremka kwa Aya.

Na twaona mfano wa hilo katika kupaka juu ya khofu mbili. Ameeleza Haatim bin Ismail, kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ali kuwa yeye alisema: (Kitabu kimezitangulia khofu mbili).

Ikrima alieleza kutoka kwa Ibin Abbas alisema: (Kitabu kimezitangulia khofu mbili) na maana yake ni kuwa lau imetokea kwa Mtume muda fulani katika maisha yake, akipaka juu ya khofu mbili, Kitabu kimekuja kinyume chake kikiinasikhi Sunna kiliposema: yaani pakeni juu ya ngozi sio juu ya viatu wala si juu ya khofu wala soksi .5

## 3. Dola Kueneza Kuosha

Watawala walikuwa wameng'ang'ania kuwa miguu ioshwe mahali pa kupaka na walikuwa wanawalazimisha watu hivyo badala ya kupaka kwa sababu ya uchafu wa chini ya nyayo mbili, na kwa kuwa kiasi kikubwa miongoni mwao walikuwa waendao miguu mitupu bila viatu, wakapenda nafsini mwao kubadilisha kupaka kwa kuosha. Na hilo lajulishwa na baadhi ya habari zilizokuja ndani ya matamko rasmi.

Ibn Jariri alieleza kutoka kwa Hamid, alisema: "Musa bin Anasi alisema hali sisi tuko kwake: Ewe Abu Hamza, kwa hakika al'Hujaaju alituhutubia akiwa Ah'wazi hali sisi tu pamoja naye akasimulia kuhusu tohara, akasema: Osheni nyuso zenu na dhiraa zenu na pakeni baadhi ya sehemu ya vichwa vyenu na sehemu ya miguu yenu, kwani hapana kitu kwa mwanadamu kilicho karibu mno na uchafu wake kuliko nyayo zake mbili, hivyo basi osheni chini yake na juu yake na kano zake mbili.

Anasi akasema:

(Mungu amesema kweli na al'Hujaju amedanganya, Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema: (na pakeni baadhi ya vichwa vyenu na baadhi ya miguu yenu na kano zake mbili. Alisema: Na Anasi alikuwa akipaka nyayo zake mbili akiziloweshe.

Na linaloweka wazi kuwa propaganda za dola zilikuwa zinaunga mkono kuosha, na humuadhibu asemaye kupaka, kiasi kwamba wasemaji wa kupaka walikuwa na hadhari kudhihirisha itikadi zao, walikuwa hawasemi waziwazi bali kwa kujificha, (dalili juu ya hilo) riwaya ya Ahmadi bin Hambali kwa sanadi yake kutoka kwa Abu Maliki al'Ash'ariy kuwa aliiambia kaumu yake: "Jikusanyeni nikuswalisheni Swala ya Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)"

Na walipokusanyika, alisema: “Je katika ninyi kuna mmoja yeyote ambaye si katika ninyi:?” Wakasema: “Hapana, isipokuwa mtoto wa dada yetu.” Akasema: “Mwana wa dada wa kaumu ni katika wao.” Akaagiza bakuli ndani yake mna maji, alitawadha na akasukutuwa na kupandisha maji puani, aliosha uso wake mara tatu na dhiraa zake mbili mara tatu tatu, na akapaka sehemu ya kichwa chake na juu ya nyayo zake mbili, hatimaye alisali.”

Hii ni mitazamo mitatu yawezekana kwayo kuosha kukahalalishiwa mahali pa kupaka pamoja na Kitabu kitukufu kujulisha kupaka. Na wa karibu mno ni wa pili kisha wa tatu.

## Aamilu Ni Nini Katika Kauli Yake (Wa-Arjulakum )?

Kwa hakika Aya ya wudhu ni dalili iliothibitishwa juu ya kuwajibika kwa wudhu na namna yake. Nayo ni Aya iliyo wazi iliteremka ili kubainisha nini lazima kwa mwenye kuswali kabla ya Swala. Na hali ya mambo yalaz- imu Aya maalumati zake ziwe wazi.

Dalili yake iwe thabiti, bila ya kuzungukwa na (maana) ya jumla jumla au utata, amesema (s.w.t.):

Na kuainisha moja kati ya kauli mbili kati ya kupaka miguu miwili au kuiosha kwafungika kwenye kumpambanua *Aamilu* katika tamko Ufafanuzi wake: Kwa kweli katika Aya tukufu kuna *Aamilu* wawili na vitenzi viwili, kwa mtazamo wa kwanza (utaona) kila moja yafaa iwe ndio *Aamilu* katika kauli yake: , isipokuwa maneno yapo katika kuain- isha *Amilu* ni nini kwa mujibu wa usafi wa kiarabu?

Na *Aamilu* hao wawili ni:

Lau tukisema: Kwa hakika *Aamilu* ni wa kwanza itakuwa wajibu miguu miwili ioshwe. Na kama tutasema *Aamilu* ni yule wa pili itakuwa wajibu ipakwe. Hivyo basi kiwajibishi ni kimoja kati ya hao *Aamilu* wawili walio kizuwizi cha kumuainisha *Aamilu* katika

Bila shaka mtazamo makini katika Aya, pamoja na kuweka kando fikra ya kila rai zilizopita na kitendo kilichoenea kati ya Waislamu, wathibitisha kuwa wa pili, yaani ndio *Aamilu* wala sio wa kwanza wa mbali. Ukipenda waweza sema: Kwa hakika Imeungwa juu ya (*ma'amulu*) wa karibu, yaani vichwa sio juu ya wa mbali, nakusudia: nyuso, na twafafan- ua hilo kwa mithali ifuatayo:

Endapo tutamsikia msemaji akisema:

(Nampenda Zaid na Omari, na nimempita Khalid na Bakari, bila ya kutia irabu kwa kusema: kwa *nasbu* (litamkwe Bakaran) au kwa *jarri* (Bakarin), tutahukumu kuwa (Bakari) ameungwa (Khalid). Na *msababishaji* wake ni kitenzi cha pili, na wala si *hajaungwa* (Amri) ili ahesabike *Aamilu* kuwa ni kitenzi cha kwanza.

Wanavyuoni wa Kiarabu wamesema kuwa haki ya *kiunganish*8 iwe kwa wa karibu sio wa mbali, na hiyo ndio asili na kuiacha (asili hii) ishara yahi- tajika katika usemi, kama si hivyo pengine husababisha utata

na kuchanganya lililokusudiwa na lisilokusudiwa.

Hebu tufanye mfano: Raisi atoe agizo kwa mhudumu wake. Mkirimu Zaid na Amri na mpige Bakari na Khalid. Yeye atapambanua kati ya jumla mbili, na ataona kuwa (Amru) ameungwa na (Zaid). Na kuwa (Khalid) ameungwa (Bakari) wala fikrani mwake halitozunguka wazo kinyume na hilo.

Ar–Raziy amenena:

Inajuzukuwa itenganishwa Aamilu wa nasbu katika kauli yake: (*arju– lakum*) ile kauli yake:

(*imsahuu*) na inajuzu iwe kauli yake (*fagh'siluu*) lakini Aamilu wawili wakikutana kwa maamuli mmoja huwa kumtendea kazi Aamilu wa karibu ndio bora.

Kwa ajili hiyo imekuwa wajibu awe Aamilu wa nasbu katika kauli yake (*arjulakum*) ni kauli yake (*wamsahu*).

**Maelezo:** Kwa ajili ya wasomaji wetu wasiopitia lugha ya Kiarabu: *Aamilu ma'amulu* katika kiarabu neno au jina herufi yake ya mwisho huwa inaka– biliwa na mabadiliko kwa mfano jina Muhammadun wakati mwingine huja Muhammadan na mwingine Muhammadin.

Na hupatikana mabadiliko haya kwa sababu. Hivyo basi msababishaji aliyelifanya hilo jina lipate haya mabadiliko ndiye aitwaye *Aamilu*. Na *maamulu* ni: Ni lile jina lililokubali mabadiliko.

Katika jumla ya kwanza tamko Muhammadu limeishia du kwa *dhumma* kwa sababu ya kutanguliwa na kitenzi *Akala*, kwa hiyo *akala* ndio *Aamilu*.

Jumla ya pili: *Ra'aytu Muhammada* hapa limekuwa na *fat'ha* kwa sababu ya kutanguliwa na kitenzi *Ra'aytu*. Hivyo basi *Ra'aytu* ndio *Aamilu.*

Mfano wa tatu: *Marartu bi Muhammadi*. Muhammadi hapa limekuwa na *kasra* kwa sababu ya kutanguliwa na *bi* kwa hiyo *bi* ndio *Aamilu*.

*Ma'amulu*: Ni aliyetendewa, mfano wa jumla hii: *Ra'aytu Muhammada*, hivyo basi *Ra'aytu*: ni Aamilu, Muhammada: ni *Ma'amulu* .

Kwa hiyo imethibiti kuwa kauli yake: (*wa arjulakum*) kwa kunasibisha *laamu* yaani kutia *fat'ha* kwawajibisha *mas'hu* (kupaka)9

Hali ikiwa kama hivyo haifai kutoka nje ya utaratibu katika mifano ya busara, maneno ya Bwana Mwenye enzi ni bora mno yawe hivyo. Wala mfano hauishii kwenye mfano tulioutaja, bali wewe waweza kuleta mifano mbali mbali ilimradi tu iwe yashabihiana na ulio katika Aya.

Lau utaileta Aya hii kwa Mwarabu halisi aliyejiweka nafsi yake mbali na madhehebu anayojiambatanisha nayo, na umuulize kuhusu dalili ya Aya atakujibu: Kuna viungo ambavyo ni wajibu kuviosha, navyo ni

nyuso na dhiraa, na kuna viungo ambavyo ni wajibu vipakwe, navyo ni vichwa na miguu.

Lau utamgeuza mtazamo wake aangalie kwenye kanuni za lugha ya Kiarabu utamuona hatangitangi (kusema) kuwa *Aamilu* wa (*ru'usi*) vichwa na (*arjuli*) miguu ni kitu kimoja nayo ni kauli yake: (*famsahuu*) wala haitozunguka mawazoni mwake fikira ya kutenganisha kati ya (*ru'usu*) vichwa na miguu, awe *Aamilu* katika vichwa ni kauli yake: (*fagh'siluu*).

Na endapo dalili ya Aya itakuwa wazi kuihusu mojawapo kati ya kupaka na kuosha, hatutahitajia kitu kingine, kwa kuwa atakayeafiki atatilia nguvu madhumuni ya Aya, na atakaye khalifu atajaribu aina ya njia ambazo iliyo bora katika hizo ni kuwa imenasikhiwa na Kitabu.

## Qira'a Mbili Na Kupaka Juu Ya Miguu

Kwa kweli kutofautiana kwa wasomi katika tamko (*wa arjulakum*) kwa fat'ha na *jarri* hakuathiri kitu kuhusu dalili ya Aya kuwa yawajibisha kupaka, kwa kuwa aina hizi mbili za usomaji zinaafikiana na kauli ile (ya kupaka) bila ya mushkeli wowote.

Ufafanuzi wa hilo: Kwa hakika Naafiu na Ibin Aamiru na Aaswimu wameisoma kauli yake (s.w.t.) (katika riwaya ya Hafsa: (*wa arjulakum*) kwa *nasbu – fat'hah* – na huu ndio usomaji ulio maarufu ambao upo ndani ya misahafu iliyoenea katika kila zama na kila kizazi.

Na Ibin Kathir, Hamzah na Abu Amri na Aaswimu wameisoma katika riwaya ya Abu Bakr kwa *jarri.* – *kasra*.

Na sisi tunasema: Kwa kweli usomaji aina mbili unawiana na kauli ya kupaka bila ugoigoi wala kutaradadi.
Ama ya pili, yaani usomaji wa *jarri – kasra* – nayo ni ushahidi wenye nguvu wa kuwa miguu imeungwa juu ya kauli yake: (*biru'usikum*) kwa kuwa soma hii ya *jari – kasra* haina sababu ila ni kuwa imeungwa na (tamko) la kabla yake.

Na hapo miguu inakuwa imehukumiwa kupakwa bila ya shaka. Ama usomaji wa *nasbu* sababu katika hilo ni kuwa kuunga kwa kufuata mahali pa (*biru'usikum*) kwa kuwa ni *mansubu mahalan* yaani mahali pa *maf 'uli* kwa kauli yake: (*wamsahu*) kwa hiyo miguu pia inahukumiwa kupaka tu. Na kuatifia mahali ni jambo lililoenea katika lugha ya Kiarabu, na pia imekuja katika Qur'an tukufu.

Ama kuhusu Qur'an amesema (s.w.t.):

"Kwa hakika Mungu ni mwenye kuepukana na washirikiina na Mtume wake – mwenye kuepukana nao" kwani usomaji (*warasuluhu*) kwa *dhumma* ni usomaji ulio maarufu ulioenea, na hakuna sababu ya kuisoma kwa *dhumma* ila ni kwa kuwa imeungwa kwa kufata mahali pa *ismu inna*. Nakusudia: *Laf 'dhuljalalah* katika kwa kuwa ni *mubtadau*.

Maswala ya kuunga kwa kufuata yamejaza vitabu vya irabu, kiasi kwamba Ibn Hisham amefanya mlango mahususi wa *atfu alal'mahali* na ameeleza sharti zake.

Ama katika fasihi ya kiarabu ielezee – *atfu alal'mahali*– hapana taabu. Msemaji amesema:

Hivyo basi usemi wake (*walalhadiida*) kwa *nasbu at'fu ala mahali* kwa kuwa ni *khabari* ya *laysa* katika usemi wake (*falasna*). Kwa hiyo tumefikia natija ifuatayo: Kwa kweli kutofautiana kwa usomaji huu wa namna mbili hakuathiri kitu kuainisha kauli ya kupaka, somo la usomaji huu wa namna mbili litaku– fikia kikamilifu kuihusu kauli ya kuosha.

Kisha ni kwamba kundi la wanataaluma wajulikanao wa Kisunni wamesema wazi kuwa Aya yajulisha kupaka, wakisema kuwa kauli yake (s.w.t.) (*wa arjulakum*) imeunganishwa na *Aamilu* wa karibu sio wa mbali, na kwamba *Aamilu* hapa ni (*famsahu*).

Na twataja baadhi ya maneno hayo:

Ibn Hazmi amesema: Ama kauli yetu kuihusu miguu miwili kwa kweli Qur'an imeshuka na kupaka, amesema (s.w.t.): (*wamsahu biru'usikum waarjulakum*), sawa iwe imesomwa kwa kutia *kasra lamu* au kwa kuitia *fat'ha*, hali yoyote iwayo ikiwa imeungwa na *ru'usi* itakuwa ima ni kufuata tamko au kufuata mahali, wala si kuhusu kinyume na hivyo.10

Ar–raziy amesema: "Ama usomaji wa *jarri* kasra walazimu miguu iwe imeungwa na vichwa, kwa hiyo kama ilivyowajibika kupaka kichwani basi ni hivyo hivyo miguuni. Ama usomaji wa *nasbi*, pia wamesema wawajibisha kupaka.

Hivyo ni kwa sababu kauli yake: (*wamsahu bi ru'usikum*) iko mahali pa nasbi, ila tu imekuwa na kasra kwa sababu ya kuingiwa na *ba'u*, kwa hiyo miguu kuiunganisha na vichwa itakuwa ruhusa katika miguu kuwa na *nasbi* ikiwa imeungwa kwa kufuata dhahir, na huu ni mwendo wa wananahau mashuhuri.

Na Sheikh Sindiy al–Hanafiy amesema: baada ya kukata shauri kuwa kwa kweli dhahiri ya Qur'an ni kupaka – na hii ndio tamko lake:

Kupaka kumekuwa ndio dhahiri ya Qur'an, kwa kuwa usomaji wa *jarri* ni dhahiri katika hilo – la kupaka – na usomaji wa nasbu yachukuliwa kwa kuifanya kuunganisha kwa kufuata mahali.11

Na huenda kadiri hii ya nukuu yatosha kubainisha kuwa usomaji wote wa namna mbili zote utatilia mkazo kupaka tu na kuambatana nako bila ya mushikeli.

## Usomaji Wa Namna Mbili Na Kuosha Miguu

Kwa kweli umejua kuwa tofauti ya usomaji katika kauli yake: (*wa arju–lakum*) haiathiri usemi wa kupaka miguu miwili sawa tuisome kauli yake (*wa arjulakum*) kwa nasbu yaani fat'ha au tuisome kwa *jarri–kasra*, soma hizo mbili zote zinatilia nguvu wajibu wa kupaka, na yafuatia kuwa *Aamilu* katika kauli yake:

(*arjulakum*) ni ile kauli yake: (*famsahuu*) na tamko (wa *arjulakum*) limeungwa na (*biru'usikum*) aidha kwa tamko au mahali.

Maneno yapo katika uwezekano wa kuitekeleza kauli ya kuosha kulingana na usomaji wa namna mbili uliyo maarufu na kadiri ya kulingana kwake na soma hizo na kanuni za lugha ya kiarabu.

Na itabainika kupitia somo hili kuwa kulazimisha kuosha kwa mujibu wa Aya hii ni ukiukaji ulio dhahiri wa kanuni za kiarabu, na ubainifu unakujia:

## Kuosha Na Usomaji Wa Nasbu (Fat'ha)

Ikiwa tutasema Aya ni dalili ya kuosha miguu, hapana budi *Aamilu* atakuwa kauli yake katika jumla iliyotangulia (*fagh'silu*) na iwe imeungwa na kauli yake: (*wujuhakum*) na hii yalazimu kutenganisha kati ya *ma'atufu* ambaye ni (*wa arjulakum*) na *maatufu alayhi* (*wujuhakum*) na jumla ngeni nayo ni (*wamsahu biru'usikum*) hali ikiwa hatenganishwi kati ya *maatufu* na *maatufu–alayhi* hata na (tamko la) neno moja sembuse jumla mzima ngeni! Wala haijasikika katika maneno ya Kiarabu fasaha msemaji aseme: kwa kuunga (Umaran ala Zaidan).

Ibn Hazmi amesema:

Haifai kuiunga *arjulakum* na *wujuhakum*, kwa sababu si ruhusa izuilike kati ya *ma'atufu* na *maatufu–alayhi* na jambo lingine jipya12

2–Abu Hayyani amesema: Na mwenye kusema kuwa usomaji wa nasbu katika (*arjulakum*) kuwa ni *kuunga kwa kufuata* kauli yake: (*fagh'silu wujuhakum wa aydiyakum*) na akatenganisha kati yao na jumla hii ambayo ni kauli yake: (*wamsahuu biru'usikum*) ni mbali, kwa kuwa kufanya hivyo ni kuweka mtengano kati ya *at'fu* na *ma'atufu –alayhi n*a jumla ya insha13

3–Sheikh Al–Halabiy kuihusu tafsiri ya Aya hii amesema: *Nasbu* (*wa arju– lakum*) ni kwa ajili ya mahali na *jarri* yake ni kwa ajili ya tamko. Na wala si ruhusa iwe *nasbu* kwa ajili ya kuunga juu ya *wujuhakum* kwa sababu ya mwanya kati ya *maatufu* na *maatufu–alayhi* kwa jumla ngeni nayo: (*wamsahu biru'usikum*), na kimsingi wasitenganishwe kati yao hata kwa neno moja sembuse jumla. Wala haijasikika katika lugha fasaha mfano wa:

Nimempiga Zaid na nimempita Bakari na Amri kwa kumuunga Amri na Zaid!14

Na Sheikh As–Sindiy amesema: "Na kuichukulia kisomo cha nasbu kwa kuunga kwa kufuata mahali ni karibu mno kwa sababu ya kufuatana kwa matumizi ya (*atfu alaa–mahali*) juu ya mahali, pia matumizi hayo yana sababu ya kujiepusha kuingiza mwanya wa neno geni kati ya, *maatufu* na *maatufu–alayhi*, kwa hiyo imekuwa dhahiri ya Qur'an kupaka.

Na15 yasiyo kuwa hayo miongoni mwa maneno yanayobainisha kuwa usomaji wa *nasbu* na kuelewa kuwa wajibu ni kuosha unalazimu kukiuka kanuni ya sarufi ya kiarabu.

### Kuosha Na Usomaji Wa Kasra

Kwa kweli wanaosema kuosha miguu wamehalalisha usomaji wa *nasbu* kwa sura ambayo umeujua udhaifu wake, na kutokuwa na uwiano na sarufi ya Kiarabu.
Lakini waliposimama juu ya usomaji wa *jarri*, na kwamba wenyewe wajulisha wajibu wa kupaka sio kuosha wameduwaa katika kuhalalisha na kuuelekeza itolewe kauli ya kuosha, kwa kuwa usomaji wa jarri uko wazi kuwa tamko (*waarjulikum*) limeungwa na ( *bi ru'usikum*) kwa hiyo hukumu yake inakuwa hukumu ya *ru'usi*), hapo basi walinepa, 'kulia kushoto' ili wapate kwa ajili ya usomaji wa *jarri* pamoja na kauli ya kuosha kihalalishi, nacho si kingine ila usemi wa kuwa hiyo jarri ni kwa sababu ya *jiwari* yaani ukaribu.

Na matokeo: kuwa tamko lake(*wa arjulakum*) limehukumiwa nasbu kulin– gana na sarufi kwa kuwa limeungwa juu ya kauli yake: (*wujuhakum*), laki– ni limejipatia irabu ya *jarri* kutokana na kauli yake: (*biru'usikum*) kwa sababu limekuwa pembezoni mwa tamko ambalo ni *majururu* na hii ndio isemwayo (*aljarru biljiwari*) yaani tamko lililoambukizwa jarri kwa sababu ya ujirani, nako ni kuliacha tamko mbali na irabu yake ya asili na kuchukua irabu ya tamko la jirani yake.

Na wametolea mfano kwa kauli yao:kwa kuwa kauli ni khabari ya kauli ya: lakini limesomwa kwa *jarri* kwa sababu ya kuwa kwake pembezoni mwa kauli kwa kuwa ni *maj'ruru* kwa kuwa ni *mudhwafu ilayhi.*

Na kwa kuwa *jarri* ya ujirani kawaida huwa haiwi katika lugha fasaha, na endapo itakuwa kwa mfano, huwa ni kwa kutimiza sharti, na hapa sharti zimekosekana. Tutatoa ufafanuzi katika mlango ufuatao.

## Kutia Kasra Kwa Ukaribu Kusihi Na Sharti Zake

Madamu wasemaji wa kuosha miguu wanatafsiri usomaji wa *jarri* kwa ujirani, hapa tunatoa maneno ya wanazuoni wa fasihi ili ieleweke umbali wa kufaa kwa matumizi ya jarri ya ujirani, na lau itakuwa sahihi, ni zipi sharti zake?

Az–Zujaju amesema: "Huenda ikasemwa kuwa (wa *arijulikum*) ni *majruru* kwa ajili ya ujirani, yaani kwa sababu ya kuwa pembezoni mwa *arru'usi* iliyo *majruru*, mfano wa kauli ya msemaji: *Juh'ru dwabi kharbi,* kwani (*kharbi*) ni khabari ya (*al'juh'ru*) kwa hiyo ni lazima iwe *mar'fuan*, lakini imekuwa *majruru* kwa ajili ya ukaribu. Hivi, halafu amepingwa kwa kauli yake: Na hiyo sio sahihi, kwa sababu ya kuafikiana wanazuoni wa lugha ya kiarabu kuwa irabu ya ukaribu ni irabu isio ya kawaida na ni ya nadra. Na (irabu) ambayo hali yake huwa hivi haifai kuichukulia Qur'an bila ya dharura inayolazimisha hilo.

Alaud–Diini Al–Bugh'dadiy amesema ndani ya tafsiri yake iitwayo '*Al– Khazinu'*: "Ama mwenye kuifanya *laamu* iwe na *kasra* katika (*al'arjuli*) kwa sababu ya ukaribu wa tamko sio hukumu. Na wamelitolea dalili kwa kauli yao: (*Juhru dwabbi kharbi*) na akasema: *Alkharbu* ni sifa ya *Al'juhru* sio ya *Adwabbi*, ila tu imechukua irabu ya *Adwabbi* kwa ukaribu, si sahihi kwa sababu mbili:

a. Kwa kuwa kasra ya ukaribu hutumika kwa sababu ya dharura ya kiushairi, au hutumika

unapopatikana usalama wa kutochanganya (maneno), kwa kuwa *Alkharbi* haiwezi kuwa sifa ya *dwabbi* – fisi – bali ni ya *Aljuh'ru* (*shimo*).

b. Na kwa sababu *kasra* ya ukaribu huwa bila ya *wau* ya kuunga, ama pamoja na *wau* ya kuunga Waarabu hawajasema.16

Asyrafiy na Ibni Jiniy wamepinga *kasra* ya ukaribu na wameifanyia taawili kauli yao (*kharbi*) kwa *jarri* – yaani *kasra*, kwa kuwa ni sifa ya Adwabbi, fisi. Na mwenye kutaka ufafanuzi na arejee Al–Mugh'niy.17

Ibn Hisham amesema: "*Jarri* ya ukaribu haiwi pamoja na herufi ya kuunga kwa sababu herufi ya kuunga inazuwia kukurubiana."

Muhtasari wa maneno ambayo tumeyanakili kwa ufupi ni mambo yafuatayo:

**Kwanza:** Kuwa *kasra* ya ukaribu haijathibiti katika usemi fasaha.

**Pili:** Kuwa kasra ya ukaribu endapo itathibiti kwa mfano, itakuwa aidha kwa sababu ya dharura ya kiushairi au kwa sababu ya kufanya uzuri chapa inayofanana kati ya matamko mawili yaliyo karibu. Na sababu mbili hizi hazipo kwenye maudhui hii. Hapa hakuna dharura ya kiushairi wala kuifanya vizuri chapa katika kulitoa tamko (*wa arjulikum*) mbali na irabu yake halisi na kulipatia irabu ya jirani yake.

**Tatu:** Kuwa kuunga kwa ukaribu kunafaa mahali ambapo kuna usalama wa kutogubikwa na tuhuma kama ilivyokuja katika mfano ulio maarufu kwa kuwa (*kharbi*) ni sifa ya shimo sio ya fisi japo itiwe kasra, kinyume na mahali hapa kwa kuwa usomaji wa *jarri* wasababisha tuhuma, lau ingekuwa miguu kwa ukweli imehukumiwa kuoshwa, kwa hiyo kuitia *jarri* kwa ujirani kwaleta tuhuma kuwa miguu imehukumiwa kupakwa na kwamba yenyewe imeungwa na vichwa bila ya msemeshwa kuwa na wazo la kuwa *jarri* hii ni ya ukaribu, hapana haja ya kuifanya aina hii ya *jarri* ambayo dhahiri yake inapingana na makusudio ya msemaji.

**Nne:** Jarri ya ukaribu haijathibiti ila katika sifa, badali, na mfano wake sio katika kiungwa kama ilivyo katika Aya. Kutokana na utafiti huu imedhihiri kuwa usemi wa kupaka unaambatana na kila moja ya soma hizi mbili bila ya hata chembe ya tafsir wala taabu, hii ni tofauti na kauli ya kuosha, kwani kauli hiyo haiwiani si na usomaji wa *nasbi*–(fat'ha) wala ya *jarri* (*kasra*).

## Ijitihadi Kuikabili Tamko La Kisheria

Kwa kweli maafa ya fiq'hi ni kushikamana na itibari na sababu za mapendekezo ili kulikabili tamko la kisheria, kwa kuwa yakinza madhehebu ya *taabudiy* – kujitoa. Kwa kuwa Muislamu anaitii (*Nassu*) tamko la kisheria – afikie afikako – haitangulizi rai yake mbele ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Kitabu na Sunnah ndio *t*ako la kisheria*,* na Sunna sahihi za Mtume wake(s.a.w.w.) (ndio *Nassu* pia), na hiyo ni alama ya kusalimu amri kwa Mwenyezi Mungu na kwa Mtume wake na Kitabu chake na Sunna zake. Amesema (s.w.t.):

Yaani msitangulie mbele ya Mungu na Mtume wake kwa kulazimisha rai zenu kwa Mtume na umma wa kiislamu. Kwa sababu kutanguliza sababu za mapendekezo mbele ya tamko rasmi ni kutangulia mbele ya Mungu na Mtume wake. Yenye neema ni yale aliyoyasema Imamu Shafiy:

“Mwenye kufuata mapendekezo atakuwa amefanya sheria”.

Si mmoja katika masunni walio mashuhuri waliofahamu kuwa dhahiri ya Aya au uwazi wake ni kupaka miguu miwili, na hilo wamelitambua kwa dhamira zao au kwa ndimi zao na kalamu zao. Lakini kutii madh’habu za maimamu wanne na wengine kumewazuwia wasiichukuwe malengo ya Aya. Hivyo basi wakafuata madh’habu zilizorithiwa badala ya kuifuata Qur’an Tukufu.

Lau wao wasingekulia na fikra hii tangu uchanga wa kucha zao, wasingezitanguliza maoni yao mbele ya Kitabu kitukufu cha Mungu kijulishacho kupaka, na wangezikomboa fikra zao kutoka vifundo vya ufuasi. Kwako kinakujia namna ya kitu fulani kutoka maoni kama haya ambayo akili hairidhiki wala dhamiri iliyo huru.

## Kuosha Kwaingiza Ndani Yake Kupaka

Al–Jaswasu amedhania kuwa Aya ya wudhu ina maana ya jumla hivyo basi hapana budi hadhari (*ih’tiati*) ifanywe, nayo ni kuosha ambako ndani yake kuna kupaka pia, kinyume na kupaka, kwa kuwa ndani yake hakuna kuosha, kisha ameondoa kitendawili cha Aya kwa madai ya kuafikiana wote kuwa lau akiosha atakuwa faradhi ameitekeleza.[18]

Izingatiwe Kwanza ni kwamba vipi ameisingizia Aya kuwa ina maana ya *ijmalu* hali ikiwa na dalili ya wazi, kwa kuwa iko katika kubainisha nini wajibu juu ya wanaoswali wote wakati wanapotaka kuswali, katika mfano kama huu inabidi iwe yenye kubainisha mradi wa Aya, isiyotazamiwa kuwa na maana ila moja. Isipokuwa tu kilichomfanya aseme *ijimalu* ni kuikimbia dhahiri ya Aya ijulishayo kuwa wajibu wa miguu ni kupaka sio kuosha.

Pili: Kwa kweli asemalo, eti kuosha ndani yake kuna kitu kupaka na wala si hivyo kinyume chake, kwa kuwa hakuna kuosha. (usemi) huu si sahihi, kwa sababu mradi wa kuosha katika maana yake ya maudhui ni kutiririsha maji juu ya kiungo, kama ambavyo mradi wa kupaka ni kupitisha mkono juu ya kiungo kwa umajimaji uliobaki mkononi, hapo basi kuosha na kupaka huwa faradhi mbili tofauti, kwa namna ambayo kila moja iko tofauti na nyingine, si kuosha imo ndani ya kupaka wala kupaka ndani ya kuosha.

Tatu: Madai ya kuondoa utata wa Aya kwa kuwa akiosha atakuwa ametekeleza faradhi yake kwa maafikiano ya wote ni mswada wa litakiwalo, kwa kuwa vipi anadai maafikiano juu ya hilo hali ikiwa wasemao kupaka kati ya Swahaba na Taabiina, majina yao yatakujia, si wachache kuwalinganisha na wasemao kuosha kama ambavyo Imamia nao ni robo ya Waislamu wote wanaona kuosha ni batili na kupaka ni lazima, sasa u–wapi huo muwafaka wa wote juu ya kuosha!

## Sunna Kukinasikhi Kitabu

Kuna ambaye aionaye Aya wazi yajulisha kupaka na yuaibatilisha kauli isemayo kuwa miguu yenu imeungwa juu ya kauli yake: (*wujuhakum*) na anasema: Haifai kabisa kuwe na kizuizi cha habari ambayo si ya maatufu kati ya maatufu na maatufu alayhi, kwa kuwa hivyo husababisha utata na kufunika na ni kupotosha si kubainisha. Huwezi ukasema:

(Nimempiga Muhammad na Zaid na nimempita Khalidi na Amri), hali ikiwa wewe kimsingi wataka kusema umempiga Amri aslan. Na Sunnah ilipokuja na amri ya kuosha miguu miwili imekuwa sahihi kuwa kupaka miguu kumeondolewa19

Izingatiwe kwanza: Kuwa haifai kuondoa hukumu ya Kitabu isipokuwa kwa Sunna iliothibiti, kwa kuwa Kitabu ni dalili iliyothibiti huku yake haiondolewi ila na dalili iliyothibiti mfano wake.

Ama hapa Sunna inayoonyesha kuosha inapingana na Sunna inayoonyesha kupaka. Vipi iwe yawezekana moja kati ya dalili mbili zinazopingana itan– guilizwe mbele kuliko Qur'an tukufu bila sababu yenye uzito?

Zitakujia riwaya zinazoungana mkono zionyeshazo kuwa Mtume (s.a.w.w.) na swahaba wake walikuwa wanapaka miguu badala ya kuosha.

Pili: Umma umeafikiana kuwa Sura ya Al–Maidah ni ya mwisho kuteremka kwa Mtume (s.a.w.w.) na kuwa haikuondolewa hukumu hata Aya moja kutoka humo. Na riwaya zimepita na kauli nyingi za swahaba zionyeshazo hivyo.

Tatu: ilimlazimu Ibni Hazmi aifanye Aya iwe dalili ya haikuondolewa hukumu kwa Sunah, lau ingethibiti kuwa Mtume aliosha miguu yake muda fulani katika umri wake basi Aya ndiyo yenye kuondoa huku ya Sunna sio kuwa Sunna imeinasikh Qur'an.

## Zinduo Kuwajibika Kuwa Mwangalifu Wakati Wa Kumwagia Maji

Zamakhshari alifahamu kuwa usomaji wa *jarri* wamlazimisha mtu aipake miguu sio kuiosha, akawa katika lengo la kuizuia dalili, na kwamba miguu ingawaje imeatifiwa juu ya vichwa pamoja na hivyo uungaji unakosa dalili ya kuosha, alisema:
Jamaa wamesoma (*wa arjulakum*) kwa *fat'ha* ikawa imejulisha kuwa miguu ya kuoshwa.
Ukisema: Utafanya nini na usomaji wa *jarri* na huingia katika hukumu ya kupaka?

Nitasema: Miguu ni miongoni mwa viungo vitatu vya kuoshwa, huoshwa kwa kumiminia maji juu yake, kwa hiyo kukawa na dhana ya kufanya israfu iliyokatazwa, hivyo ikaungwwa kwenye kiungo cha tatu kinachopakwa sio kwa sababu ipakwe (miguu) bali kutanabahisha kuwa matumizi ya wastani ni wajibu wakati wa kumiminia maji juu yake, na imesemwa mpaka nguyu mbili

Izigatiwe kwanza: Kuwa sababu alizo zisema zitasihi tu ikiwa nukta ni ile ielewekayo na wasemeshwa

wote katika waumini, mbali walioje na nukta hii ambayo Zamakh'shariy ameibuni akielekeza kwenye madh'hebu yake! Kwa ibara nyingine: Nukta aliyoisema itakuwa sahihi endapo itakuwa salama mbali na kugubikwa na utata, si katika nafasi ambayo haina usalama huo.

Na yafuatia lichukuliwe tamko la dhahiri kuwa kupaka ni wajibu, ighafilikiwe nukta adhimu ya Sheikh Zamakh'shariy!

Pili: Mikono pia ni mahali pa kudhaniwa israfu kama miguu, basi ni kwa nini hakutanabahisha wajibu wa matumizi ya wastani katika kumwagia maji mikono pia?!

Hayo yote yanadhihirisha kuwa sababu hizi ni njia ya kuwaelekeza watu kwenye madh'hebu ambayo Bwana wa Al-Kashaafu amekulia na kama si hivyo haingemjia moyoni mwake sababu hii.

## Urahisi Wa Kuosha Miguu Miwili Si Kama Vile Nywele

Ibin Qudaama alipofahamu kuwa muktadha wa kuatifia *al'arjuli ala ru'usi* ni *al'mas'hu kupaka*, sawa isomwe kwa *nasbu* au kwa *jarru*, hapo akaan- za kuleta falsafa na kufanya jitihada kuikabili dalili iliyo thabiti na akasema: "Kuna tofauti kati ya kichwa na mguu, na kwa mujibu huo hai- wezekani viwili hivyo vihukumiwe hukumu moja, na sababu ni:

1. Kinachopakwa kichwani ni nywele ambazo huwa taabu kuziosha, na miguu miwili ni kinyume na hivyo kwa hiyo hiyo yashabihiana mno na vioshwavyo.

2. Kwamba miguu miwili ina mpaka huishia hapo kwa hiyo yashabihiana na mikono miwili.

3. Kwamba miguu miwili iko kwenye hatari ya kuchafuka kwa kuwa hukanyaga kwayo ardhini kinyume na kichwa.

**Izingatiwe:** Kuwa ni ijitihadi binafsi katika kulikabili tamko rasmi la sheria na kutia falsafa katika hukumu.

Ama (hoja) ya kwanza: Hivi kuna mashaka gani katika kuosha nywele endapo kioshwacho kikiwa sehemu ya hizo nywele, kwa kuwa ndio wajibu katika kupaka, basi na iwe hivyo wakati wa kuosha.

Ama ya pili: Kushikilia hoja ya kushabihiana ni hoja dhaifu sana kwa kuwa vingi vilioje vishabihianavyo vyatofautiana katika hukumu. Na sababu ilio fasidi mno kuliko hiyo ni ile ya tatu, kwa kuwa miguu miwili kuwa kwake katika hatari ya kuchafuka hailazimu kuainishiwa kuosha, kwa kuwa ase- maye kupaka anasema kuwa ni wajibu miguu iwe tohara kisha ipakwe.

Kwa umri wangu, hakika sababu hii na iliyotangulia ya Zamakhshariy ni kuichezea Aya kwa lengo la kuyaunga mkono madhehebu. Linalopendeza kwa mwana fiq'hi mwerevu ni kuifanyia kazi Aya, sawa iafikiane na mad- hehebu ya Imamu wake au hapana. Na bwana wa tafsiri Al-Manar ana neno la maana sana kuwahusu hawa wanaotanguliza fatwa za maimamu kuliko Kitabu kitukufu na Sunna sahihi, asema: "Kwa kweli kufanya amali kwao ni kwa kulingana na kauli za vitabu vyao mbali na kitabu cha

Mungu na Sunna za Mtume wake.

## Kuwafuata (wanazuoni) waliopita katika kuosha

Ibin Taymiyya alipofahamu kuwa usomaji wa kasra yalazimu kuiunga miguu na (hukumu ya) vichwa na italazimu kuipaka miguu miwili sio kuiosha, alikimbilia kulifanyia tafsiri 'tamko rasmi la kisheria, na akasema: "Na mwenye kusoma kwa *kasra*, maana yake si (*wamsahu arjulikum*) pakeni miguu yenu) kama wanavyodhania baadhi ya watu, kwa sababu kadhaa, moja yake:

Kwa kweli waliosoma hivyo katika salafu,–walio tangulia –walisema: amri limerudi kwenye kuosha."20

**Izingatiwe:** Kuwa endapo yatakuwa sahihi aliyoyasema italazimu isemwe kuwa Salafu waliiacha Qur'an nyuma ya migongo yao na wakayachukuwa yasiyoafikiana na Qur'an. Lau kurejea kwao kutakuwa kwa ajili ya kuon– dolewa hukumu ya Kitabu, umekwishajua kuwa hukumu ya Qur'ani haindolewi na khabari ya *Aahadi*. Na hata tukikubali kuwa kuinasikhi ni jaizi, haijaondolewa hukumu yoyote kutoka katika Sura ya Al–Maidah.

Na miongoni mwa ajabu ni kuwa Ibni Taymiyya amejikinza mwenyewe, amesema katika sababu ya saba, hii ndio *nassu* ya usemi wake: Arabic text (*inna tayammuma juila badalan minal wudhui indal haadja fahudhifa shatru a'adhwail'wudhui wa khufa ash shatru thaani, wadhalika fainnahu hudhifa ma kana mamsuhan wa musiha makana magh'sula*.)21

(Kwa kweli tayammamu imefanywa badala ya udhu wakati wa haja, hivyo basi vimefutwa nusu ya viungo vya udhu na kufanywa wepesi nusu ya pili, na hivyo vimefutwa vilivyokuwa vikipakwa na kupakwa vilivyokuwa vikioshwa).

Kama tayammamu msingi wake utakuwa kufuta kilichokuwa kikipakwa itakuwa hukumu ya miguu imefutwa katika tayammamu, hivyo italazimu hukumu yake iwe kupaka ili iwe sahihi kuifuta, na lau itakuwa hukumu yake ni kuosha itakuwa haikufutwa, itabaki kama uso na mkono na hupakwa!

## Kuiwekea Mpaka Aya Ya Kuosha

Kwa hakika mfasiri maarufu kwa jina la Sheikh Ismail Haqiy Al– Burusawiy ameunga mkono kauli ya kuosha kwa sababu kupaka hakujaeleza mpaka ila tu kuwekewa mpaka kumekuja katika viungo vioshwavyo.

Kwa maneno yake haya anakusudia kuwa miguu imewekewa mpaka wa ka'abu mbili kwa hiyo kuosha ka'abu mbili kumeshabihiana na mikono iliyowekewa mpaka wa viwiko. Kwa hiyo yahukumiwa kuoshwa kwa hukumu ya ushirika katika kuwekewa mpaka.

**Izingatiwe:** Kuwa kila moja kati ya vioshwavyo na vipakwavyo katika Aya vimekuja na mpaka na bila ya mpaka. Kwa hiyo nyuso katika Aya huoshwa wala haukuwekwa mpaka, na mikono huoshwa na mpaka umewekwa kwa kauli yake: (*ilalmarafiqi*) hivyo basi yajulikana kutokana na hali hiyo kuwa kuosha

pengine huwa na mpaka na pengine bila ya mpaka, hivyo basi mpaka sio dalili ya kuwajibika kuosha wala kukosa mpaka sio dalili ya kuwajibika kupaka, na hali ni hiyo kwenye kiungo kipakwacho, kwani miguuu kulingana na ilivyochaguliwa – hupakwa na huwa na mpaka, ni mpaka kwenye kaabu mbili, na kichwa hupakwa nacho.

## Udhuu Kwa Mtazamo Wa Qur'ani Na Sunna

hakina mpaka. Hivyo basi kuifanya mipaka ndio alama ya kuosha yafanana mno na kuifanya *a'am* kuwa ni dalili ya *akhasu*.

Na alilosema kuwa katika kupaka haukuja mpaka wowote, maneno ameyafanyia ta'awili ni sawa na kuyafanya madai ndiyo dalili.

Lau tukisema kwa kuzizingatia pendekezo kama hizi, kwa mujibu wa uzuri wa lugha yalazimu miguu iwe yenye kupakwa si kuoshwa.

Al'Murtadha amesma: "Kwa hakika ndani ya Aya muna utajo wa kiungo cha kuosha kisichowekewa mpaka nacho ni uso, na kime'atifiwa au kuungwa na kiungo cha kuoshwa chenye mpaka nacho ni mikono miwili, kisha ikaanzwa kutajwa kiungo kipakwacho kisicho kuwa na mpaka nacho ni kichwa, basi ni wajibu miguu iwe ya kupakwa nayo imewekewa mpaka na imeungwa si viungo vingine, ili jumla mbili zikabiliane katika kuungwa kinachooshwa chenye mpaka juu ya kioshwacho kisicho kuwa na mpaka, na katika kuungwa kipakwacho chenye mpaka juu ya kipakwacho kisicho na mpaka22

## Rejea Ni Sunna Endapo Aina Mbili Za Usomaji Zitapingana

Madh'habu ya Alusiy ni kuwa aina mbili za usomaji zilizozagaa zenye kupingana zinakuwa kama Aya mbili zinazopingana, na asili ifuatwayo katika mfano kama huu ni kuzidondosha zote mbili na kurejea kwenye Sunna!

Amesema: "Kwa hakika aina mbili za usomaji zilizozagaa kwa ijimai ya makundi mawili, bali kwa itifaki ya Waislamu wote, na miongoni mwa kanuni za Usuli kwa makundi mawili kuwa aina mbili zilizozagaa za usomaji endapo zitapingana katika Aya moja, zitakuwa na hukumu ya Aya mbili, hapana budi kwetu tufanye juhudi na kujitahidi kwanza kuziowanisha kwa kadiri iwezekanavyo. Kwa sababu asili ya dalili ni kuzitendea kazi sio kuzitelekeza kama ilivyokubalika kwa wana usuli, baada ya hapo tutafute ya kuitilia uzito kati ya mbili hizo, na endapo haikutuwia wepesi kuitilia uzito tutaziacha na kuelekea kwenye dalili zingine katika Sunna.

**Izingatiwe:** Ni miongoni mwa ajabu kujalia visomo viwili kuwa zinapingana baada ya hapo tufanye juhudi kuondoa upinganaji kwa njia ambazo msemaji amezisema, kwa sababu kujaalia mfano wowote wa kupingana kati ya aina mbili za usomaji ni rehani ya kuzusha dhehebu katika Qur'an na kulitendea kazi, kama si hivyo basi visomo viwili havina upingano wala (hakuna cha) kudondoshwa, hivyo vyote viwili zinalenga jambo moja nalo ni kupaka miguu miwili, kwa kuwa kauli yake (s.w.t.): (*wa arjulakum*)

visomo hivyo vyote viwili vimeungwa na tamko moja nalo ni kauli yake: (ru'usikum) lakini ima ni *atfu* juu ya mahali kwa hiyo hufanywa *nasbu* yaani *fat'ha* au kuungwa kwa kufata tamko kwa hiyo hufanywa *jarri kasra*.

## Kuosha Ni Nyongeza Ya Mtume (S.A.W.W.)

Jamalud Dini Al-Qasimiy anasema kuwa Aya iko wazi kuwa fardhi ni kupaka kama alivyosema Ibnu Abbas na wengine, lakini kuitilia maanani kuiosha miguu miwili katika *Ma'athur* ni kuizidisha katika fardhi na kuipanua kulingana na kawaida yake, kwa kuwa yeye amefanya katika kila faradhi Sunna inayoiunga na kuipa nguvu katika Swala, Zaka, Saumu, na Hijja.

Na miongoni mwa yajulishayo kuwa wajibu wake – miguu – ni kupaka ni kule kufanywa kwa sheria ya kupaka juu ya khofu mbili na socksi, nalo halina sanadi ila ni Aya hii. Kwa kuwa kila Sunna asili yake ni ndani ya Kitabu cha Mungu kwa matamshi au kwa inavyofahamika. Jua hivyo na hifadhi na Mungu ndio mwongozi.23

**Izingatiwe:** Mtume (s.a.w.w.) ameepukana na sifa ya kuzidisha au kupun- guza katika faradhi, bali yeye amefuata wah'yi na kaulimbiu yake ilikuwa:

(***Qul innama atabiu maa yuhaa ilayya min Rabbiy***) (***Al'A'araf: 203***).
(Sema: Mimi ni mwenye kufuata wahyi tu kutoka kwa Mola wangu) na kauli yake:

(***Qul ma yakunu liy an ubadilahu min tilqai nafsiy in atabiu ila maa yuuha ilayya***) ***10:15***
(Sema sikuwa niibadilishe itakavyo nafsi yangu sifuati isipokuwa wahyi ufikao kwangu).
Lau azidishe (kitu) katika swala ni kwa amri kutoka kwa Mungu (s.w.t.).

Kisha lau atazidisha azidishacho huzidisha ambacho kimethibiti asili yake kwa Sunna, sio kwa Kitabu kitukufu kama kuongeza rakaa mbili kwenye swala za rakaa nne na rakaa katika swala ya rakaa tatu.

Muslim ametoa (habari) kutoka kwa Ibin Abbas, alisema: Mungu alifarad- hisha Swala kupitia ulimi wa Mtume wenu (s.a.w.w.) nyumbani rakaa nne na katika safari rakaa mbili. (*Sahih Muslim*, juzuu ya 2, uk.143) *Babu Swalatul-Musafiriyna.*
Lau tufanye mfano kuwa faradhi ilikuwa kupaka si kuosha na kwamba Mtume (s.a.w.w.) amezidisha kwenye faradhi kwa hukumu ya riwaya zina- zoamrisha kuosha, lakini tutafanyaje sasa na riwaya zinazoamrisha kupa- ka, nazo ni riwaya sahihi nyingi kama itakavyokujia kikamilifu, je hapa kuna kimbilio baada ya kupingana ila ni Kitabu kitukufu?!

Na maneno haya yote yanabainisha kuwa wafuasi wa riwaya hizi walichukuwa msimamo mapema mukabala wa Aya zinazoeleza na zenye dalili za wazi, na kulazimisha madhehebu yao juu yake (hizo Aya), jambo ambalo limewaingiza katika mbabaiko, matatizo na katika azma, na waligonga milango yote ili watoke humo na walijiangika na sababu za mapendekazo yasiyofaa.

## Kushikamana Na Masilahi.

Bwana wa 'Manaar' alipotambua kuwa maana dhahiri ya Aya ni kupaka juu ya miguu kwa mkono uliolowa kwa maji, alijaribu kuitoa Aya mbali na maana yake ya dhahiri kwa kushikamana na maslahi, na alisema: "Haiingii akilini hekima yoyote kuwajibisha kupaka juu ya unyayo kwa mkono uliolowa, bali ni kinyume na hekima ya wudhu, kwa sababu kulowana kiasi kidogo kukiingia juu ya kiungo ambacho kina vumbi au uchafu kwazidisha uchafu, na mkono wa mpakaji unapata sehemu ya uchafu huo.

**Izingatiwe:** Alilosema ni miongoni mwa mapendekezo, hayategemewi ikiwa tamko la kisheria lipo, wala hapana shaka kuwa hukumu za kishe– ria zinafuata maslaha ya kweli, wala si wajibu juu yetu kujuwa undani wake. Hivyo (kwa mtizamo wetu kibinadamu) kuna masilahi gani katika kupaka juu ya kichwa hata kwa kadiri ya kidole au vidole viwili, kiasi kwamba mpaka (Imamu) Shafiy amesema:

(*Idha masahar ra'asa bi'iswibain wahidatin au baadhi iswibain au ba'a– tini kaffihi, au amara man yamsahu lahu, ajza'ahu dhalika ?!*–

(Endapo atapaka kichwa kwa kidole kimoja au baadhi ya kidole au kwa sehemu ya ndani ya kitanga cha mkono wake, au akamuamuru atakayem– paka litamtosha hilo!

Na kuna neno la maana la Imamu Sharafud–dini Al'Musawiy, twalileta tamko lake hapa. Amesema: "Sisi tunaamini kuwa mfanya sheria mtakatifu aliwaangalia waja wake katika kila alichowakalifisha nacho miongoni mwa hukumu zake za kisheria, wala hakuwaamuru isipokuwa lenye maslahi kwao. Na wala hakuwakataza ila ambalo lenye ufisadi na ndani yake lina uovu kwao.

Lakini yeye (s.w.t.) pamoja na hayo hakujaalia chochote miongoni mwa uwezo wa kutambua hukumu hizo uwe umepimwa kulingana na maslahi na uovu kwa mujibu wa rai za waja, bali kutii kwao kuwe kwa dalili zenye nguvu alizowaainishia, hakuwafanyia mwanya wa kuelekea kingine.

Na ya kwanza miongoni mwa dalili hizo za hekima ni Kitabu cha Mungu Mtukufu, naye amepitisha hukumu ya kupaka vichwa na miguu katika udhu, hivyo hakuna upenyo wa kuacha kukiri hukumu yake. Ama usafi wa miguu kwakuwa mbali na uchafu hapana budi uhifad– hiwe kabla ya kupaka juu yake kulingana na dalili mahsusi zilizojulisha kuwa tohara ni sharti kwenye viungo vya wudhu kabla ya kuanza wudhu.24

## Kuingia Kati Jumla: (Famsahu..) Ni Kwa Ajili Ya Kubainisha Utaratibu

Kwa hakika kufanya mwanya kati ya herufi ya kiungo "na" "??" kwa kauli (f*amsahu biru'usikum*) ni kwa ajili ya kubainisha kutangulia kupaka kabla ya kuosha miguu.25

**Izingatiwe:** Msemaji ana nafasi ya kukusanya kati ya kuitaja taratibu na uwazi wa kubainisha kwa kukariri kitenzi kwa kusema:

Kwa hiyo yanakuwa maneno yake yamejengeka kulingana na makusudio yake na wakati huo huo yako

safi bila ya utata.

## Kupaka Juu Ya Miguu: Katika Hadith Sahihi

Kwa hakika umetambua – kutokana na dalili ya Aya – kuwa faradhi maha– la pa miguu ni kupaka, na kwa sababu Aya iliteremka mwisho mwisho wa maisha ya Mtume na hazijaondolewa hukumu bado, kwa hiyo zenyewe binafsi ni dalili tosha juu ya lililokusudiwa.

Isipokuwa kwa ajili ya kutilia nguvu makusudi, sisi tutataja yaliyoelezwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) na kutoka kwa maswahaba wake kuwa yalazimu kupaka juu ya miguu, na kwa hilo twafupisha kwa kuonyesha yaliyo kwenye matni peke yake pamoja na kujiepusha na sanadi, kwa sababu risala hii haina nafasi ya kuzitaja (sanad).

### Yaliyoelezwa Kutoka Kwa Mjumbe Wa Mwenyezi Mungu Kuhusu Kupaka Miguu

1. Kutoka kwa Bisru bin Sa'id alisema: Alimpelekea Uthmani kigoda akaomba maji, alisukutua na kuvuta maji puani kisha aliosha uso wake mara tatu na mikono yake mara tatu tatu na alipaka sehemu ya kichwa chake na miguu yake mara tatu tatu, hatimaye alisema:

(*Ra'aytu Rasulallahi* (*s.a.w.w.*) *hakadha tawadhwa'a yaa haaulai'a kadhalika? Qaaluu: Na'am, linafarin min as'haabi Rasuulillahi* (*s.a.w.w.*)26

"Nilimuona Mtume wa Mungu akitawadha kama hivi, oh ninyi, ndivyo? Walisema: Na'am, kwa watu miongoni mwa maswahaba wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)."

2. Kutoka kwa Hamrani alisema: Uthmani aliomba maji akatawadha kisha alicheka, hatimaye alisema: "Hamuniulizi nacheka nini?" Wakasema: "Ewe Amiirul'muuminna kitu gani kimekuchekesha?"Akasema: "Nimemuona Mtume wa Mungu akitawadha kama nilivyotawadha, alisukutua na kupandisha maji puani na aliosha uso wake mara tatu na mikono yake mara tatu na alipaka sehemu ya kichwa chake na juu ya unyayo wake."27

3. Na katika *Musnad* ya Abdullahi bin Zaid Al–Maazniy kuwa Mtume (s.a.w.w.) alitawadha na aliosha uso wake mara tatu na mikono yake mara mbili na alipaka kichwa chake na miguu yake mara mbili.28

4. Kutoka kwa Abu Matar alisema: Wakati sisi tumeketi pamoja na Ali msikitini, alikuja mtu kwa Ali na alisema: "Nionyeshe wudhu wa Mtume (s.a.w.w.)." Alimwita Qambar, na alisema: Niletee kimtungi cha maji, akaosha mikono yake na uso wake mara tatu, aliingiza baadhi ya vidole vyake kinywani na alipandisha maji puani mara tatu, na aliosha dhiraa zake mbili mara tatu na alipaka kichwa chake mara moja na miguu yake miwili mpaka ka'abu mbili hali ndevu zake zinatona kifuani mwake hatimaye alikunywa funda moja baada ya wudhu kisha akasema:

Muulizaji wa wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) yu wapi? Ni kama hivi ulivyokuwa wudhu wa

Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)."29

5. Kutoka kwa Ubbadu bin Tamim, kutoka kwa baba yake, amesema: "Nimemuona Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) alitawadha na alipaka kwa maji juu ya ndevu zake na miguu yake."30

6. Kutoka kwa Ali bin Abi Talib (a.s.) alisema: "Nilikuwa naonelea kuwa chini ya nyayo mbili ndiko kunastahiki kupakwa kuliko juu yake mpaka nilipomuona Mjumbe wa Mungu anazipaka juu yake."31 Kutoka kwa Rufa'ata bin Raafi'i kuwa yeye alimsikia Mjumbe wa Mungu (s.a.w.w.) akisema:

(*Annahu la yajuzu swalatu ahadikum hata yasbaghal'wudhua kama ama- rahu llahu azza wajalla,thumma yagh'silu wajhahu wayadayhi ilal'mir- faqayni, wayamsaha ra'asahu warijlayhi ilalka'abayni*)32

(Kwamba Swala ya mmoja wenu haitojuzu mpaka akamilishe wudhu kama Mungu Mtukufu alivyomuamrisha, kisha aoshe uso wake na dhiraa zake mbili pamoja na mirfaqi mbili – viwiko viwili na apake kichwa chake na miguu yake miwili mpaka ka'ab mbili."

7. Yaliyoelezwa kutoka kwa Abdullahi bin Amrin, alisema: "Alichelewa mbali na sisi Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) katika safari tulioisafiri, alitudiriki hali Swala imetupita nasi twatawadha tukawa tunapaka juu ya miguu yetu, akanadi kwa sauti yake ya juu kabisa:

(*way'lu lil'a'aqabi minannari*)(ole wa nyayo na moto) mara mbili au tatu.33

8. Kutoka kwa Abu Maaliki Al'Ash'ariy kuwa aliiambia kaumu yake: "Jikusanyeni niwaswalisheni Swala ya Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)."

Walipojikusanya, alisema: "Je kati yenu kuna ambaye si katika ninyi?" Wakasema: "Laa, isipokuwa mtoto wa dada yetu." Akasema: "Mtoto wa dada wa kaumu ni miongoni mwao." Akaagiza bakuli ndani yake muna maji, akatawadha na akasukutuwa na kupandisha maji puani, akaosha uso wake mara tatu na dhiraa zake mbili mara tatu, na alipaka sehemu ya kichwa chake na juu ya nyayo zake mbili, hatimaye aliwaswalisha, alifanya takbir nao ishirini na mbili."34

9. Kutoka kwa Ubaadu bin Tamim Al-Maazniy, kutoka kwa baba yake kuwa yeye alisema: "Nilimwona Mjumbe wa Mungu akitawadha na ana- paka maji juu ya miguu yake miwili."35

10. Kutoka kwa Ausi bin Abiy Ausi Athaqafiy kuwa yeye alimuona Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) alikuja kwenye mfereji wa kaumu huko Twaifu, alitawadha na alipaka juu ya nyayo zake.36

11. Kutoka kwa Rufa'ata bin Raafi'u alisema: Nilikuwa nimeketi kwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) punde mtu mmoja alimjia aliingia msikitini akaswali na alipomaliza swala akaja na kumsalimu Mjumbe wa Mungu (s.a.w.w.) na kaumu ya waliokuwa na Mjumbe wa Mungu, hapo akasema Mtume wa Mungu ( s.a.w.w.): (*Irja'a fa swali fa innaka lam tuswal*) Rejea ukaswali kwa kuwa haujaswali) yule mtu akawa anaswali, nasi tukawa tunaiangalia Swala yake hatujui kinachoitia dosari, na alipokuja na kumtolea

salamu Mtume (s.a.w.w.) na ile kaumu ya watu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: (*wa alayka irji'i fa swali fainnaka lam tuswali*) (yakupasa urejee ukaswali kwa kuwa haujaswali).

Hammaam alisema: "Hatujui kama alimwamuru kufanya hivyo mara mbili au tatu." Yule mtu alisema: "Sijui kilichoitia dosari swala yangu?"Akasema mjumbe wa Mungu (s.a.w.w.): "Kuwa Swala ya mmoja wenu haitimii mpaka akamilishe wudhuu kama Mungu alivyomuamuru, aoshe uso wake na mikono yake miwili mpaka viwiko vyake viwili na apake sehemu ya kichwa chake na miguu yake na ka'ab zake mbili, hatimaye asome tak'biiratul'iharam na amsifu Mungu, kisha asome Sura ya Al–fatihah na anayoijuwa na kuwa rahisi, kisha asome takbiira na afanye rukuu, aweke vitanga vya mikono yake juu ya magoti yake kiasi cha kutulia viungo vyake na vitulie kisha aseme: *Samia llahu liman hamidah,* na asimame sawasawa mpaka ausimamishe mgongo wake na kila mfupa uchukuwe nafasi yake, halafu asome takbiira na asujudu aumakinishe uso wake."

Hammamu alisema: "Huenda alisema paji lake la uso ardhini mpaka maun– gio yake yatulie na kupumua kisha asome takbiira na akae sawasawa kwa makalio yake na kuusimamisha uti wa mgongo wake.

Aliielezea Swala kama hivi mpaka alimalizia rakaa nne, halafu alisema: "Swala ya mmoja wenu haitotimia mpaka awe amefanya hivyo."37

12. Kutoka kwa Ibn Abbas yeye alisema: "Kulielezwa kupaka juu ya nyayo mbili mbele ya Umar na Sa'ad na Abdullah bin Umar. Umar bin Al– Khattab alisema: "Sa'd ni mwanachuoni zaidi kuliko wewe." Umar alisema: "Ewe Sa'd kwa kweli sisi hatupingi kuwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) alipaka – yaani juu ya nyayo mbili–lakini je, alipaka tokea ilipoteremshwa Suratul–Maaidah, kwa kuwa (hiyo) imeimarisha kila kitu na imekuwa Sura ya mwisho katika Qur'an isipokuwa Baraa'ah."38

13. Kutoka kwa Urwa bin Zubair kuwa Jibraiyl (a.s.) alipoteremka kwa Mtume (s.a.w.w.) mwanzo wa bi'itha alizibua chemchem ya maji huko al'Ijaazi alitawadha na Muhammad (s.a.w.w.) yuamwangalia; aliosha uso wake, na mikono yake mpaka viwiko viwili na alipaka baahi ya kichwa chake na miguu yake mpaka kaabu mbili. Na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alifanya kama alivyomuona Jibrail anafanya.39

14. Abdur Rah'man bin Jubair bin Nufair alieleza kutoka kwa baba yake kuwa babe Jubairi alikuja kwa Mtume (s.a.w.w.) akiwa na binti yake ambaye alimuoa Mjumbe wa Mungu, Mtume wa Mungu aliagiza chombo cha maji akaosha mikono yake miwili aliinadhifisha, kisha alisukutua mdomo wake na kupandisha maji puani, halafu aliosha uso wake na mikono yake miwili mpaka viwiko viwili mara tatu, kisha alipaka kichwa chake na miguu yake.40

Mpaka hapa yametimia tuliyogundua katika riwaya kutoka kwa Mtume Mtukufu (s.a.w.w.) kwa sura ya mpito, nazo zaonyesha kuwa kauli ya Mtume na kitendo chake ilikuwa ni kupaka sio kuosha.

## Yaliyoelezwa Kutoka Kwa Maswahaba Na Taabi'ina Kuhusu Kuosha Miguu

15. Sufian alituhadithia alisema: "Nilimuona Ali (a.s.) alitawadha akapa- ka juu (ya nyayo) mbili."41

16. Kutoka kwa Hamrani kuwa yeye alisema: "Nilimuona Uthman akiagiza maji ya kutawadha, akaosha vitanga vyake mara tatu na alisukutua na kupandisha maji puani na aliosha uso wake mara tatu na dhiraa zake mbili mara tatu na alipaka baadhi ya kichwa chake na juu ya nyayo zake."42

17. Aaswimu'al-Ah'walu kutoka kwa Anasi alisema: "Qur'an ilishuka na kupaka na Sunna (ilishuka) na kuosha. Na isnadi hii ni sahihi."43

18. Ikrimah, kutoka kwa Ibn Abbas alisema: "Wudhu ni (sehemu) mbili za kuosha na mbili za kupaka."

19. Abdullah al-Aatkiy, kutoka kwa Ikrimah alisema: Si wajibu kuiosha miguu miwili imeteremka kuihusu kuipaka."

20. Kutoka kwa Jaabir kutoka kwa Abii Jafar Al'Baaqir (a.s.) alisema: "Paka juu ya kichwa chako na nyayo zako mbili."

21. Kutoka kwa Ibn Alyata bin Daudi, kutoka kwa Aamir Asha'abiy kuwa yeye alisema: "Ni kupaka juu ya miguu miwili, huoni (sehemu ambazo) zilikuwa wajibu kuosha zimefanywa wajibu kupaka na ambazo zilikuwa wajibu kupaka zimetelekezwa (katika tayammumu)."

22. Kutoka kwa Aamiru Ash'shaabiy, alisema: "Vimeamriwa vipakwe katika tayammamu ambavyo viliamriwa vioshwe katika udhu, na ame- batilisha alivyoamrisha vipakwe katika wudhu: Kichwa na miguu miwili."

23. Kutoka kwa Aamiru Ash'shqaabiy alisema: "Vimeamrishwa vipakwe kwa mchanga katika tayammumu (viungo) vilivyoamrishwa vioshwe kwa maji na kutupiliwa mbali vilivyoamrishwa kupakwa kwa maji."

24. Yunus alisema alinihadithia ambaye aliyefuatana na Ikrima mpaka Waasiti alisema: "Sikumuona akiosha miguu yake, bali alikuwa akiipaka juu yake mpaka aliporudi kutoka huko."

25. Qutadah katika kutafsiri kauli yake (s.w.t.):

(*fagh'silu wujuhakum wa aydiyakum ilalmarafikqi wamsahuu biru'usikum wa arjulakum ilal'kaabayni*) na osheni nyuso zenu na dhiraa zenu mpaka viwiko, na pakeni baadhi ya vichwa vyenu na miguu yenu mpaka kwenye ka'ab mbili). Mungu amefaradhisha (sehemu mbili za) kuosha na mbili za kupaka.

26. Musa bin Anas alimwambia Abiy Hamza kuwa Al'Hujaju alituhutubia huko Ah'wazi tukiwa pamoja naye, alitaja *atwahuuru* akasema:

*Igh'silu wujuhakum wa aydiyakum wamsahu biru'usikum wa arjulakum*, na kwamba hapana kitu kwa

mwanadamu kilicho karibu mno na uchafu wake kuliko nyayo zake, basi osheni chini yake na juu yake na kano zake mbili.” Anas akasema: “Mungu amesema kweli na al-Hujaju amesema uwongo, amesema Mungu (s.w.t.) (*wamsahu biru'usikum wa arjulakum*).

Alisema: “Na Anas alikuwa aoshapo miguu yake huilowanisha.” Amesema Ibn Kathiir: Isnaadi yake ni sahihi.[44]

27. Ash'Shaabiy alisema: “Jibril aliteremka na kupaka, kisha Ash'Shaabiy alisema: huoni kuwa mwenye kufanya tayamumu yampasa apake aliyokuwa akiosha na[45] aache aliyokuwa akipaka.”[46]

28. Ismail nilimwambia Aamiru ash'Shaabiy: Kuwa watu wanasema kuwa Jibril aliteremka na kuosha miguu miwili? Akasema: “Jibril aliteremka na kupaka.”[47]

29. Nizaalu bin Sabrah kuwa Ali aliomba maji akatawadha kisha alipaka juu ya ndara zake na nyayo zake. Hatimaye aliingia msikitini alivua viatu vyake kisha akaswali.[48]

30. Abiy Dhwabian alisema: “Nilimuona Ali akiwa na shuka ya rangi manjano na kishali na mkononi mwake kuna mkuki alikuja kwenye shamba la Asajin kisha alichepuka alitawadha na alipaka juu ya ndara zake na nyayo zake hatimaye aliingia msikitini, na akavua ndara zake kisha akaswali.[49]

Hii ni nyembamba kutoka nene na kidogo kutoka kingi, kwa mwenye kupekuwa sanadi nyingi na *Sihahi* na majaamiu ya Aathaar ataelewa mengi kuliko tulioelewa kwa njia ya mpito.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۖ فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ ۗ{90}

***“Hao ndio ambao Mungu amewaongoa hivyo fuateni muongozo wao.”* (*Al-An'aam: 90*).**

## Kupuuza Riwaya Za Kupaka

Kwa kweli amezipuuza Ibn Kathir na waliomfuata riwaya za kupaka na alisema: Rawafidhu wamekhalifu hilo (kuosha miguu miwili) bila ya egemeo, bali kwa ujahili na upotovu, kwakuwa Aya tukufu yajulisha wajibu wa kuosha miguu miwili pamoja na ilivyothibiti kwa *tawatur* tendo la Mtume (s.a.w.w.) kwa kuafikiana na ilivyojulisha Aya tukufu, na wao wanakwenda kinyume na hayo yote,
na wala hawana dalili iliyo sahihi katika suala lenyewe.[50]

Kana kwamba hakuizingatia kwa makini Aya tukufu na uwazi wa dalili yake juu ya kulazimika kupaka, na kana kwamba hakuzielewa hizo Hadith nyingi alipodai kuwa kuna *tawatur* katika kuosha, au alielewa lakini hakuzizingatia.

Na sheikh Ismail Al-Burusawiy amemfuata akisema: “Rawafidhu wanaitakidi kuwa la wajibu kuihusu

miguu ni kupaka, na wamezieleza habari (riwaya) dhaifu zisizo za kawaida kuhusu kupaka."51

Na hivyo hivyo amedai Al-Alusi, Shia wamejiangika na riwaya moja: alisema wala hawana hoja katika madai ya kupaka ila riwaya walioitoa kwa Ali (*Karamallah Taala Wajihahu*)

(*innahu masaha waj'hahu wa yadayhi, wa masaha ra'asahu warijlayhi, washariba fadhla twahurihi qaiman*).52

Hata ikiwa al-Burusawiy na al-Alusiy wamesamehewa kwa udhuru katika dhana hii, na iwe hakuna dalili ya kuwajibisha kupaka isipokuwa riwaya zisizo za kawaida, basi hawatokuwa na udhuru waliozielewa riwaya hizi nyingi ambazo ni zaidi ya riwaya thelathini, hata kama hatutosema kuwa kupaka kumenakiliwa kwa tawatur itakuwa hapana budi tuseme kuwa ni nyingi.

Ongeza juu ya hivyo kuwa Kitabu kinaiunga mkono, hivyo basi sisi hatuna njia isipokua tuchukuwe ambacho Kitabu kinaafiki, na kuifanyia tafsiri ili – riwaya – ambayo iendayo kinyume nacho, yaani inayojulisha kuosha kwa namna fulani, kwa kusema: Alikuwa akiosha muda baada ya bi'itha lakini Aya tukufu ilifuta – hukumu hiyo. Au tuichukulie maana nyingine (*wala taqfu ma laysa laka bihi ilmun*). (Usifuate ambalo hauna elimu nalo).

## Majina Ya Swahaba Na Tabiina Wajulikanao Wasemao Kupaka

Bila shaka umejua riwaya zionyeshazo lazima ya kupaka katika udhu, na zimeelezwa na wajulikanao miongoni mwa Swahaba na Tabiina na wamezinakili wenye vitabu (vijulikanavyo kuwa ni *Sihahi*), na pia wenye *masaniidi*.

Ili kumjulisha msomaji majina yao na kiasi cha nafasi zao katika kunakili, twataja majina yao pamoja na kudokeza wasifu wao kwa ufupi na kuam- batanisha na namba za semi zao. Ili msomaji aelewe kuwa wasemao hivyo ni kundi la Swahaba na Tabiina na vilele vya waamininiwa:

Imam Ali bin Abi Talib (a.s,) na kuwa yeye alayhisalam alisema:

(*Lau kaana diinu bir ra'ayi la kaana baatinul'qadamayni ahaqu bil'- mas'hi min dhahirhumaa, laakin ra'aytu Rasuulallahi* (*s.a.w.w.*) *masaha dhwahirahumaa*. (Angalia Hadith 6).

Imamu Al-Baqir (a.s.) Muhammad bin Ali bin al Husayni al-Imamu athab- tu al-Hashimiy al-Alawiy al Madaniy ni mmoja miongoni mwa waju- likanao.

Ameeleza kutoka kwa baba yake, na alikuwa Bwana wa Baniy Hashim katika zama zake alikuwa mashuhuri kwa al'Baqir kwa ajili ya kauli yao: *Baqaral ilma*, yaani shaqahu, *fa alima aswilahu wakhafiyahu* (Tazama Hadith 21).

Bisru bin Said, ni Imamu Al-Qudwatu Al'Madaniy, ni maula wa Baniy Al'Hadhramiy, alihadithia kutoka kwa Uthmani bin Affan: Yah'ya bin Muinu na An-Nasaiy walimthibitisha, Muhammad bin Sa'ad alisema:

“Alikuwa miongoni mwa wanaibada wenye kujitenga na watawa, mwenye Hadith nyingi. (Angalia Hadithi ya 1).[53]

Hamranu bin Aabaanu yeye ni maula wa Uthman bin Affan, aelezea kuto- ka kwake (Angalia Hadith 2) na alikuwa miongoni mwa wanaojulikana, Ibn Habaan ameeleza kuwa ni miongoni mwa waaminiwa.[54]

Uthman bin Affani, imetangulia katika Hadithi (1 na 2) kwa kweli yeye alikuwa anatawaza na anapaka juu ya miguu yake na akisema: “Huu ni wudhuu wa Mtume wa Mungu (s.w.t.).

Abu Matar, Ibn Haban alimtaja kuwa ni miongoni mwa waaminifu, Al’Hujaaj bin Artwa’atu amechukuwa riwaya kutoka kwake (Taz. Hadith 3).

Abdullah bin Zaid Al-Maazniy mwenye Hadithi ya wudhu kutoka kwa maswahaba bora hujulikana kuwa ni Ibin Ummi Ammaratu. Ibin Habani amemtaja kuwa yu miongoni mwa wanaoaminika. (Angalia Hadithi 3).

Anizalu bin Sibra Al-Hilaliy Al’Kuufiy, ameeleza kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) na kwa Ali (a.s.) (Angalia Hadithi 30) Na Uthman, Abubakar, na Ibin Mas’ud. Al’Ajaliy amesema: “Ni Kuufiy Taabi’i, mwaminifu miongoni mwa Taabiina wakubwa. Na Ibin Habani amemtaja kuwa yu katika waaminiwa.[55]

Abdu Khayr bin Yaziid, Al’Ajaliy alisema kuwa: Ni mtu wa Kuufa Taabi’i mwaminifu. Na Ibin Haban alimtaja kuwa ni miongoni mwa waaminiwa mataabi’i Abdu Swamadu bin Sa’id Al’Himswiy amekata shauri kuwa ni mkweli muaminifu katika kitabu *As-Swahaba*. (Angalia Hadithi 6).

Ubaadu bin Tamim bin Ghaziyah al’Answariy al’Khazrajiy al’Mazniy: Ameeleza kutoka kwa baba yake na kwa ammi yake Abdullahi bin Zaid na kutoka kwa Uwaimiru bin Saadi, alimsema kuwa mkeli: al’Ajaliy na An- Nasaiy na wengine, na habari yake ndani ya As-Sahihayni (Al-Bukhariy na Muslim) na ibun Habani kuwa ni miongoni mwa mkweli (angalia Hadithi 10,5).

Abdullah bin Abbas bin Abdul Muttalib bin Hashim ibun Abdi Manaafi, alikuwa anaitwa Al-Baharu kwa wingi wa elimu yake, na aliitwa Hibrul’Ummah. Na Abdullah bin Utbah alisema: Ibin Abbas amewazidi watu kwa mambo kadhaa: Kwa elimu alizowapita, na fiq’hi iliyohitajika kutoka rai yake, na alisema: Sikupata kumuona yeyote aliyekuwa mjuzi zaidi ya kumshida katika Hadithi za Mtume wa Mungu kuliko yeye. Wala mwenye uelewa zaidi katika rai kutokana na yeye, wala mjuzi zaidi wa tafsiri ya Qur’an kuliko yeye[56] (Angalia Hadith 13,19).

Ausi bin Abiy Ausi At-Thaqafiy: Kutoka kwake As’habu Sunanu wanne wameeleza riwaya, Hadithi sahihi katika riwaya za Shamiyina kutoka kwake. (Angalia Hadithi 11).

Asha’abiy: Aamiru bin Sharahiil bin Abdi, yeye ni Imamu Al’Hafidhu, Al’Faqih, Al’Mutaqiy, ni ustaadhu wa Abiy Hanifa na ni Sheikh wake. Ahmad bin Hambali na Al’Ajaliy walisema: Hadith *mursalu* ya Asha’abiy ni sahihi, kwa sababu yeye haelezei Hadith *mursalu* isipokuwa iliyo sahi- hi. Ibin Uyainah alisema: Wanavyuoni ni watatu: Ibin Abbas katika zama zake, na Asha’abiy katika zama zake, na Athauriy katika

zama zake.[57] (Angalia Hadithi 22, 23, 24, 28).

Ikrimah: Abu Abdillah Al–Madaniy Maula wa Ibin Abbas, Ibin Haban amemtaja katika thiqaatu. Na alisema: Alikuwa miongoni mwa wanazuoni wa zama zake kwa fiq'hi na Qur'an, na Jaabir bin Zaid alikuwa akisema: Ikrima ni miongoni mwa wanazuoni, wameeleza kutoka kwake As'habu Sunanu wa nne Hadithi zilizo sahihi.[58] (angalia20, 25).

Rifaatu bin Raafiu bin Maliki bin Al'Ajalani Abu Mu'adhi Azzarqiy, ali– hudhuria Badri. Na alikuwa na riwaya kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.). Alikufa mwanzoni mwa ukhalifa wa Muawiyah. Ibin Haban alimtaja miongoni mwa waaminifu.[59] (Angalia Hadithi ya 7,12).

Urwatu bin Azzubair bin Al'Awamu Al'Qarashiy nduguye Abdullahi bin Az–Zubair, Faqiihun, Aalimun.

Na alikuwa miongoni mwa wana wa Madina waliobora na miongoni mwa wanazuoni wake. Ibin Haban amem– taja miongoni mwa waaminifu.[60] (Angalia Hadith 14).

Qutaadatu bin Azizi, Al–Haafidh, Al'Alammah Abul'Khataabi Asadusiy Al–Baswariy Adhwariru Al'Akmah Al'Mufasiru. Amesema Ahmad bin Hambal: Qutada ni mwanachuoni wa tafsiri na wa tofauti za wanazuoni. Na alimsifu kuwa ni mwenye kuhifadhi. Na alienda mbali zaidi kumueleza. Na alikuwa mwenye hifadhi mno miongoni mwa watu wa Basra. Alifariki huko Wasiti katika (Kitongoji cha Twauni) mwaka118 A.H.[61] na Ibin Habaan amemtaja kuwa ni miongoni mwa waaminifu. (Angalia Hadith 26).

Anas bin Maliki Ibn Anadhwar mhudumu wa Mtume (s.a.w.w.) alikwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) akiwa kijana wa miaka kumi, na alifariki (s.a.w.w.) naye akiwa na miaka ishirini. Alihamia Basra na alikufa huko mwaka 91 A.H. (Angalia Hadith18).

Musa bin Anas bin Maliki, Qaadhi wa Basra, anaeleza riwaya kutoka kwa baba yake. Kutoka kwake Mak'hulu na Hamiidu Atwawilu walichukua riwaya,[62] (Angalia Hadithi 27).

Husain bin Jundab al'Kuufiy al'Janbiy (Abu Dhwabyani al'Kuufiy) Anaelezea riwaya kutoka kwa Ali bin Abi Talib na Salmani. Kutoka kwake wamechukuwa riwaya: Ibrahim na al'Aa'mashi. Amekufa mwaka 56 A.H. Ibn Habani amemtaja miongoni waaminifu. (angalia Hadithi 31).

Jubayr Ibn Nufayri bin Malik bin Aamir al'Hadhramiy. Anachukua riwaya kutoka: Kwa Abu Dharr na Abu Dar da'u. Kutoka kwake wamechukua riwaya watu wa Shaam. Kuniya yake ni Abu Abdir Rah'mani, alifariki mwaka 80 A.H. huko Shaam. Ibin Haban amemtaja katika waaminifu. (Angalia Hadithi 15).

Ismail bin Abiy Khalid al'Bujaliy al'Ah'masiy Abu Abdillahi Al'Kuufiy. Al–Ajaliy amesema: Alikuwa mtu mwema mwaminifu, thabiti, na alikuwa mkosoaji. Marwan bin Muawiyah alisema: Ismail alikuwa akiitwa Al– Mizan. Alikufa mwaka 146 A.H.[63] (Angalia Hadithi 29).

Tamimu bin Zaid Al'Maazniy, Abu Ubadu Al'Answariy katika Bani An– Najaar, amekuwa Swahaba, Hadithi zake ziko na mwanawe.[64](Angalia Hadith 5,10).

At–Twau al'Qudahiy, anachukua riwaya kutoka kwa Abdillah bin Umar, na Urwa bin Qays amechukua kutoka kwake, baba yake Ya'aliy bin Atwa'u, Ibnu Haban amemtaja kuwa ni miongoni mwa waaminifu. (Angalia Hadithi 11).

Abu Maliki al'Ash'ariy: al'Harithu bin Al–Haarithi al'Ash'ariy Ash– Shaamiy Aswahabiy, ameelezea Hadithi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) na kutoka kwake Abu Salamu al'Aswadu. Kuniya yake ni Abu Maliki, na alikufa katika khilafa ya Umar. (Angalia Hadithi 9).

Kama utastaajabishwa basi ya kustaajabisha ni kauli ya Ash–Shaukaniy, aliposema: "Haikuthibiti kutoka kwa mmoja yeyote miongoni mwa swa– haba kinyume na hivyo (yaani kuosha) isipokuwa Ali na Ibun Abbasi na Anas.65

Isipokuwa itikadi yake kuhusu kuosha imemzuia kutafiti na kufuatilia katika vitabu vya Sunanu na Masaaniidu.

## Wudhu Wa Mtume (S.A.W.W.) Kutoka Usemi Wa Maimamu Wa Nyumba Ya Mtume (S.A.W.W.)

Kwa kweli Maimamu katika Ahlu–bayt ni rejeo la pili ya Waislamu baada ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuhusu walilohitilafiana (Waislamu), kwa kuwa wao ni wahifadhi wa Sunna ya Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) na ni kasha la elimu yake, kwa hakika Mtume (s.a.w.w.) ameagiza hivyo katika Hadithi ya *Thaqalayni* ambayo Waislamu wameafikiana kuinakili na usahihi wake na amesema (s.a.w.w.):

"Kwa hakika nimeacha kati yenu vitu viwili vya thamani: Kitabu cha Mungu na Kizazi changu." Ikiwa hii ndio nafasi ya Ahlu–bayt naturejee kwao kuhusu jinsi ya wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) kwa kuwa wao wamefyonza kutoka maji baridi yanayokimbia na walihifadhi Sunna ya Mtume kwa kunakili mkubwa kwa mkubwa, na hapa yanakuijia waliy– oyaeleza yakujia:

**1–** Kutoka kwa idadi kadhaa ya swahibu zetu, kutoka kwa Ahmad bin Muhammad na Abi Daudi wote kutoka kwa Husein bin Sa'id kutoka kwa Fadhwalatu kutoka kwa Daud bin Farqad, alisema: "Nilimsikia Abu Abdillah akisema: Kwa kweli baba yangu alikuwa anasema: Kwa hakika wudhu una mpaka, mwenye kuuvuka hatopata malipo. Mtu mmoja aka– muuliza: "Mpaka wake ni upi?" Akasema: "Utaosha uso wako na mikono yako miwili, na utapaka kichwa chako na miguu yako miwili."66

**2 –** Ali amenakili kutoka kwa baba yake, na kwa Muhammad bin Ismail, kutoka kwa al'Fadhlu bin Shadhani, wote kutoka kwa Hamadiy bin Isa, kutoka kwa Harizu, kutoka kwa Zurara alisema: "Abu Ja'far (a.s.): (Ala ahkiy lakum udhua Rasuulillahi (s.a.w.w.)? Qulna: Balaa.) (Je, nisikuonyesheni wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)?" Tukasema: "Ndio tuonyeshe," akaagiza chombo chenye maji kidogo, akakiweka mbele yake, halafu alipania dhiraa zake na aliingiza kiganja chake cha kulia, kisha akasema: "Ni kama hivi ikiwa kiganja kiko tohara," kisha aliteka na kukijaza maji na aliyamwagia kwenye paji la uso wake na akasema: (*Bismillah*) na aliyaeneza kwenye ncha za ndevu zake, kisha ali– upitisha mkono

wake usoni kwake na juu ya paji la uso wake mara moja, halafu alitumbukiza kiganja chake cha kushoto akateka na kukijaza, kisha alikiweka kwenye kiwiko chake cha kulia na alipitisha kiganja chake kwenye dhiraa yake mpaka maji yalitiririka kwenye ncha za vidole vyake, na alipaka mbele ya kichwa chake na juu ya nyayo zake kwa umajimaji wa kiganja chake cha kulia na baki ya umajimaji wa kushoto.

Alisema: Na Abu Ja'far alisema (a.s.): (Kwa hakika Mungu ni Witri anapenda witiri, yaweza kukutosheleza maji miteko mitatu: Mmoja kwa ajili ya uso na miwili kwa ajili ya dhiraa mbili, na kwa umajimaji wa mkono wako wa kulia utapaka kichwa na umaimaji uliobakia utapaka juu ya unyayo wako wa mguu wa kulia, na utapaka kwa umajimaji wa kushoto wako juu ya unyayo wako wa kushoto).

Zurara alisema: "Abu Ja'far (a.s.) alisema: (Mtu mmoja alimuuliza Amiirul'Muuminiina wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.). Alimuonyesha kama hivi).67

**3 –** Ali bin Ibrahim, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ibn Abiy Umair, kutoka kwa Umar bin Udhayna, kutoka kwa Zurara na Bakiir kuwa waw– ili hawa walimuuliza Abu Ja'far (a.s.) kuhusu udhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) aliagiza chombo ndani yake muna maji, aliutosa mkono wake wa kulia aliteka mjazo alimwagia usoni kwake aliosha kwa mkono huo uso wake, kisha alitosa kiganja cha mkono wake wa kushoto, kwacho aliteka mteko akamwagia kwenye dhiraa yake ya kulia akaosha kwao dhiraa yake kutoka kwenye kiwiko hadi kwenye kitanga cha mkono, haurudishi kwenye kiwiko. Hatimaye alikitosa kiganja chake cha kulia akamwagia dhiraa yake ya kushoto kutokea kwenye kiwiko, na alifanya kama alivyofanya mkono wa kulia. Halafu alipaka kichwa chake na nyayo zake kwa unyevunyevu wa kiganja chake, hakuvifanyia maji mapya, hatimaye alisema: wala asiingize vidole vyake chini ya kanda. Kisha akasema:
Kwa hakika Allah Mtukufu anasema:

(***yaa ayyuha lladhiyna Aamanu idha Qumtum ilaswalati fagh'silu wujuhakum wa aydiyakum***)***: Qur:5–6***

"Enyi mlioamini mkusudiapo kuswali osheni nyuso zenu na dhiraa zenu..."

Asiache kitu mikononi mwake hadi viwiko viwili ila awe amekiosha kwa sababu Mungu anasema:

Hamae akasema:

Hivyo akipaka kitu kichwani mwake au nyayoni mwake kati ya ka'abu mbili mpaka ncha za vidole itamtosha, alisema. "Tukauliza: Ka'abu mbili zi wapi? Akasema: "Hapa, yaani kwenye mgawanyiko (kati ya unyayo na muundi)." Tukauliza: "Hiki ni nini?" Akasema: "Huu ni katika mfupa wa muundi, na ka'ab ni chini zaidi ya hiyo."

Tukasema: "Mungu akurekibishe, choto moja latosha kwa ajili ya uso na choto kwa ajili ya dhiraa?" akasema: "Ndio likifika humo, na mawili yanakuja kwa vyote hovyo.

**4 –** Kutoka kwa idadi kadhaa ya watu wetu: Ahmad bin Muhammad, Ali bin Al'Hakam, Daudi bin An–

Nu'uman, Abu Ayyubu, Bakiir bin Ayan, kutoka kwa Abu Ja'far (a.s.)

Alisema: "Je nisiwaonyesheni wudhu wa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)," akachota kwa mkono wake wa kulia gao la maji, kwayo aliosha uso wake halafu aliteka kwa mkono wake wa kushoto gao la maji kwayo aliosha mkono wake wa kulia, halafu aliteka kwa mkono wake wa kulia gao la maji kwayo akaosha mkono wake wa kushoto, hatimaye alipaka kwa mabaki ya mikononi mwake kichwa chake na miguu yake.

## Hatima Ya Mzunguko Huu

Ukweli umebainika na kudhihiri kwa uwazi wake wote hivyo ni kwa mambo yafuatayo:
Kitabu kimesema kwa sauti ya wazi kupaka miguu na kwamba Qur'an Tukufu haiafikikuosha.

Kwa hakika kundi katika swahaba wajulikanao na vilele katika wao – ambao ni bweta la kuhifadhia Sunna na ni wahifadhi wa athari – walikuwa wakipaka na wanakataa kabisa kuosha, na nimezijua riwaya zao nyingi zinazofikia kusaidiana.

Kwa hakika Maimamu wa Ahlul–bayt, wakiwemo miongoni mwao: Maimamu wawili al–Baqir na As–Sadiq (a.s.) wamebainisha udhu wa Mtume wa Mungu, kuwa yeye alikuwa anapaka miguu badala ya kuiosha, na maneno yao yamekwishapita.

Na (dalili) zilizojulisha kuosha miguu kuna ambazo ni sahihi na dhaifu, bali dhaifu ni zaidi kuliko sahihi. Hivyo basi ni wajibu wa mwanachuoni agange kupingana kwa riwaya zinazoonyesha kuosha, kwa kuzilinganisha na Kitabu kwanza, pili kuziambatanisha na Sunna zinazoonyesha kupaka.

Kwa hakika Mtume (s.a.w.w.) ndiye aliyewaamuru Waislamu wote kuchukua kauli ya kizazi chake, aliposema: (Inniy taariku fiikum Ath thaqalayni Kitaba llahi wa Itratiy) (Hakika nimeacha kati yenu vizito viwili – vyenye thamani – Kitabu cha Mungu na kizazi changu).

Kwa hiyo kujiambatanisha na kauli zao na Hadith zao ni kutekeleza kauli ya Mtume (s.a.w.w.) naye haitoi ila kwa haki, kwa hiyo mwenye kuvichukua vyenye thamani viwili atakuwa ameshikamana na kitakachomuokoa mbali na upotovu, na mwenye kukichukua kimoja kati ya viwili atakuwa amemkhalifu Mtume.

Ukiongeza kuwa Ali (a.s.), ni mlango wa elimu ya Mtume. Yeye ni maarufu kwa kauli ya kupaka. Na Ar–Raziy anasema katika kuongoka na Ali: (wa man iqtadaa fii dinihi bi Aliyin bin Abiy Talib faqadih'tada,) na dalili juu ya hilo ni kauli yake (s.a.w.w.) (Allahuma adril'haqa ma'a Ali haythu dara.)68 (Ewe Allah izungushe haki pamoja na Ali azungukapo).

Ikiwa ijitihadu maana yake ni kuitumia juhudi katika kuichomoa hukumu kutoka dalili zake za kisharia basi ni kwa nini neema hii kubwa imekua mah'susi kwa maimamu wanne tu, na si wengine? Na vipi imekuwa waliotangulia ndio wastahiki zaidi kuliko waliokuja nyuma?

Haya na yaliyo mfano wake yalazimu kufungua mlango wa ijitihadi katika zama zetu hizi, na kuzingatia kitolewacho na Qur'an na Sunna katika hukumu za maswala haya na mfano wa haya ni miongoni mwa ambayo yatakayokupitia katika mlolongo huu, yakiwa mbali na kauli za maimamu wanne na walio mfano wao.

Kwa kweli ijtihadi ni alama ya kudumu kwa dini na kufaa kwake kulin– gana na hali ya mambo na mazingira na wala si bid'aa ya kuzushwa, bali ilikuwa wazi toka zama za Mtume na baada ya kifo chake (s.a.w.w.) na (mlango wake) ulifungwa kwa sababu za kisiasa mnamo mwaka 665 A.H.

Al'Miqriziy alisema yalipoanza kuzingirwa madh'habu kwa wanne tu: Yaliendelea mamlaka ya maimamu hao wanne tokea mwaka 665 A.H. kiasi kwamba haikubaki katika jumla ya nchi za kiislamu madhehebu ijulikanayo miongoni mwa madh'habu za kiislamu isiokuwa hizi nne, na alifanyiwa uadui afuataye madh'habu isiyokuwa hizi nne, na alikanushwa na wala kadhi yeyote hakupenda wala kukubaliwa shahada ya yeyote kama angekuwa si mfuasi wa mojawapo ya madhehebu hizi.

Na wanavyuoni wao walitoa fatwa katika nchi hizi kipindi chote cha muda huu wajibu wa kuzifuata madhehebu hizi na kuziharamisha zisizokuwa hizi, na kuzitendea kazi hizi mpaka hii leo.69

## Na Mwisho Wa Dua Yetu Ni Al'hamdulillahi Rabbi L'alamiin.

1– Aya ya wudhu ni Aya yenye mafuhumu wazi na yenye kueleweka.

2– Mwanzo wa tofauti katika wudhu.

3– Qur'an Tukufu ni msimamizi na ni marejeo pekee zinapotofautiana athari.

4 – Sura ya Al–Maaidah ni Sura iliyoteremka mwisho.

5– Chimbuko la tofauti.

6 – Nini *Aamilu* katika kauli yake (*wa arjulakum*).

7 – Aina mbili za usomaji na kupaka juu ya miguu.

8 – Aina mbili za usomaji na kuosha miguu.

9 – *Kasra* ya ujirani kusihi na sharti zake.

10 – Kujitahidi kulikabili tamko rasmi.

11 – Kupaka juu ya miguu katika Hadithi sahihi.

12 – Kupuuza riwaya za kupaka.

13 – Majina ya maswahaba mashuhuri na Tabi'ina wasemao kupaka.

14– Wudhu wa Mtume (s.a.w.w.) kutoka usemi wa maimamu Ahlulbayt (a.s.).

---

1. Sahih Muslim kwa sherehe ya An–Nawawiy: 3\115, Na. 229.
2. Sahih Muslim kwa sherehe ya An–Nawawiy: 3\115, Na. 230.
3. Mafaatiihul'ghaybi au Atafsiyrul'Kabiiru: 3\252, chapa ya mwaka1308, Misri.
4. Ad–Durul'Manthur: 3\403 .
5. 1 na 2. Nuru Thaqalayni: 1\483.
6. 1 na 2. Ad–durul'manthur: 3\1,4.
7. 1na2.2
8. At'fur: Ni kiunganishi mfano wa 'na' katika Kiswahili. K.m yaani mkirimu Zaid na Amri kwa hiyo na ndio at'fu kama vili katika kiarabu.
9. 161/11
10. 56/2:
11. 161/11
12. 56/2:
13. 558/1:
14. .16
15. .88/1
16. 16/2:
17. 1 na 2. Mughniy Alabibu, mlango wa nane,Al'qaidah Athania,359.
18. Ah'kaamul'Qur'an:2\346.
19. 510/1
20. .386/2:
21. .48/4
22. Al'intiswar:24.
23. Ata'awilu:6/112
24. Kwa minajili hiyo twaona watembeao miguu wazi miongoni mwa Shia katiyao wafanyi kazi– kama wakulima na walio mfano wao nawengine wasiotilia manani usafi wa miguu yao wakati usio wa ibada iliyo na sharti ya tohara– wakusudiapo wudhu huosha miguu yao kisha wana tawadhwa na wapaka juu ya miguu ikiwa safi na mikavu.
25. Gazeti'Alfaiswalu N0235 uk,48, maqala ya Abu Abdur rah'mani Adhahiry
26. Musnad Ah'mad:1/109, Hadith489.
27. Kanzul'ummali:9/439, Al'hadiithu26863.
28. Kanzul'ummali:9/439, Al'hadiithu26863.
29. Kanzul'umal:9 /448 kwa namba 26908.
30. Kanzul'umal:9/429 kwa NO26822
31. Musnad Ah'mad :1 N0 937 na 919
32. Sunanu Ibn Maajah:1,hadiith 460;Sunanu Annasaaiy:2\226.
33. Swahihul'Bukhariy:1\ 23, Babu man rafa'a swautahu bil'ilmi min kitabil'ilmi, Al'hadiith 1.
34. Musnad Ahmad: 5 \342.
35. Sunanu Ibin Maajah:1, Al Hadith 460.
36. Tafsiyru Tabariy: 6\86; Al–Mu'ujamu Akabir: 1\221 N0 603.
37. Mustadrakul–Hakim: 1\241
38. Mustadrakul–Hakim: 1\241
39. Al Khaswaisul Kubraa: 1 \94
40. Usudul'Ghabah: 5 \156
41. Musnad Ahmad, Al'hadiith 1018.

42. Kanzul Ummal: 5 \106.
43. Hadithi 18-26, zote zimenakiliwa kutoka Tafsiri ya Tabariy: 6 \82.
44. Atabariy: Jaamiul'bayani: 6 \182. Alqaasimiy: Mahasinu ta'awili: 6 \111;
45. Ibn Kathiiri Adamashqiy, Tafsiyrul qur'an Aladhiim:2 \27.
46. Tafsiyrul Qur'an Al'adhwimu: 2\27.
47. Tafsiyrul Qur'an Al'adhweem: 2 \25
48. Kanzul'ummal:9 \ 435 kwa N026856
49. Kanzul Ummal: 5 \ 126.
50. Tafsirul'Qur'an Al'Adhwimu: 2\518.
51. Tafsiru Ruhul'Bayani:\351.
52. Hivyo hivyo katika toleo, na sahihi ni aliosha.
53. Tadhkiratul'hufadh: 1\ 124. Tah'dhiibu tahdhiibi:9 \350, Hilyatul'auliyai:3 \ 180. Shadharatu dhahabi: 1 \ 149. Atabaqaatul kubra ya Ibin Saad: 1 \ 149.
54. Ibn Hayyani: Athiqaatu: 4 \ 179.
55. Tah'dhiibu Tahdhiibu:10\ 423; Al'Bukhariy: At-Tariykhu Al'Kabiiru:8\117
56. Usudul'Ghaabah: 3 \ 192-195.
57. Tadhkiratul'Hufaadhu: 1 \ 79,Tah'dhiibu tah'dhiibu: 5\65, Hilyatul'Auliya'I lil'Asbahaniy:4\310, Shadharatu dhahabi: 1\126, Twabaqaatul'hufadhu:43.
58. Tah'dhiibu tah'dhiibu:7\293, Tadh'kiratul'hufaadhu:1\95, Tah'dhiibul'asmaau:1\340.
59. Athiqaatu:4\240
60. Athiqaatu:5\194-195. Tadh'kiratul'hufaadhu:1\92.Tah'dhiibutah'dhiibu:7\180.
61. Athiqaatu:5\321, Albidaya wa nnihayah li ibin Kathiir:9\313. Tah'dhiibul'asma'u:2\57, Tah'dhiibu tah'dhiibu:8\337.
62. Athiqaatu:5\401.
63. Tadhkiratul' hufaadhi:1\153,, Tahdhiibu tahdhiibu:1\291. Al'abar:1\203.
64. Athiqaatu:3\41.
65. Ashaukaniy: Neilul'autari:1\163.
66. Alkulayniy: Al'kaafiy: v,3 kitabu twahara, babu twahara babu miqdarul'mai alladhi yujzyi lilwudhui wal'ghusli waman ta'ada fil'wudhui, Al-hadiith.3
67. Alkaylaniy: Alkafiy:v 3, kitabu twahara, babu sifatul'wudhui, Al'hadiith 4.
68. Ar- raziy: Mafaatiihul'ghaybi:1\111.
69. Rejea Al'khutatu al'miqriziah: 2 \333-344.

# Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na sita
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)

7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu Imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Kwa Mujibu wa Ahlul Bayt
33. Adhana kwa mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Je, Kufunga Mikono Ni Bidaa au Sunna? Kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
43. Kukusanya sala mbil

# Back Cover

**"Udhuu Kwa Mtazamo Wa Qur'ani Na Sunnah"**

Imekuwa ni kawaida ya watu kukubali kila jambo linalofanywa na watu katika jamii wanayoishi bila ya hoja yoyote; jambo hilo liwe zuri au baya. Na hii hutokana na kukaririka kwa jambo kwa muda mrefu mpaka linakuwa ni mazoea ya watu.

Hivyo inapotokea watu fulani wachache katika jamii kufanya jambo kinyume na vile walivyozoea, huwashangaa watu wale na kulikana jambo hilo bila kuchunguza uzuri au ubaya wake. Na hoja yao ni kwamba jambo hilo halifanywi na watu wengi, wanasahau kwamba wingi sio hoja.
Hoja ni maneno yaliyokamilika kielimu, kiakili na kimantiki.

Wanachuoni wa Kiislamu wanatofautiana juu ya kutawdha miguu. Wengi wa wanachuoni wa Kisunni wamejuzisha kuosha miguu, ambapo wanachuoni wa Kishia wamjuzisha kupaka. Ipi ni njia sahihi, jibu utalipata katika kitabu hiki, ambalo mwandishi amelifikia kwa kutumia Qur'an na Sunnah, vyanzo viwili ambavyo ni chimbuko la sheria na hukuma zote za dini kwa madhehebu zote za kiislamu

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
**Alitrah Foundation**
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [12]
Tovuti: www.ibn-tv.com [13]

---

**Source URL:** https://www.al-islam.org/node/25292

**Links**
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/25292%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/25292%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/sheikh-jafar-subhani
[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/person/sheikh-harun-pingili
[6] https://www.al-islam.org/library/general-laws-worship
[7] https://www.al-islam.org/tags/qur%E2%80%99
[8] https://www.al-islam.org/tags/swala
[9] https://www.al-islam.org/tags/dini
[10] https://www.al-islam.org/tags/sheria
[11] https://www.al-islam.org/person/mtume-muhammad-saw

[12] mailto:alitrah@raha.com
[13] http://www.ibn-tv.com